# Nipashe

Ijumaa Aprili 26, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579902

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Majaliwa awaelekeza ma-DC, RC vitambulisho wamachinga

UKURASA 3



Ukurasa 18

Madereva wasafirishaji mafuta nje walia kusingiziwa dhuluma

Ukurasa 19

Mtihani wa kinamama kufikia '50 kwa 50' katika ujasiriamali

Ukurasa 14

BUFE

Ijumaa Aprili 26, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

TBS ilipotua ghafla Mbeya ikaibua 'madudu' viwandani, sokoni, madukani

Ukurasa 16

Muungano unavyowashia uchumi wa Watanzania 'taa ya kijani'

KIBIASHARA ZAIDI Ukurasa 19 Madereva walia kusingiziwa dhuluma Ukurasa 18

UKURASA 13

### HOFU YA KIMBUNGA

# Serikali yatoa maagizo mazito



UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**MACHINJIO YA 980 MILIONI HAYATUMIKI**
MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amebaini kutokutumika kwa machinjio ya Nyakato jijini Mwanza ...

UKURASA WA 5

**JPM AMPA MBARAWA MWEZI KERO MAJI**
RAIS John Magufuli, amempa mwezi mmoja Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Prof. Makame Mbarawa, kuhakikisha anatatua changamoto ya maji




Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, (IGP) Simon Sirro (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, baada ya kufungua mkutano wa siku mbili wa kimataifa wa wakuu wa polisi wa nchi saba. Wengine ni Mkuu wa Polisi wa DRC, Dieudonne Amuli Bahigwa (wa pili kushoto), Mkuu wa Polisi Rwanda, Dan Munyuza (katikati) na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Robert Boaz (kushoto). **PICHA: MIRAJI MSALA**

## NDUGAI AMVAA ZITTO KABWE

UK 3

# Watumishi 190,000 kupandishwa vyeo

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA YABAKIZA 8 ZA YANGA KILELENI** UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# Machinjio yaliyogharimu mil. 980/-hayatumiki

**Na Enock Charles**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amebaini kutokutumika kwa machinjio ya Nyakato jijini Mwanza licha ya mradi huo kukamilika, ukigharimu Sh. milioni 980.989.

Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/18, Prof. Assad anabainisha kuwa mradi huo ni sehemu ya mkakati wa serikali wa kupunguza uchafuzi wa Ziwa Viktoria unaotokana na majitaka.

Anabainisha kuwa Mradi wa Maji Safi na Majitaka Awamu ya II ulitiwa saini kupitia mkataba namba ME-011/2015-16/W/05 wa jumla ya Sh. 980,988,900 kwa ajili ya ukarabati wa machinjio ya Nyakato jijini Mwanza kuanzia Julai 22, 2016 hadi Novemba 24, 2017. Katika ripoti yake hiyo, Prof. Assad anabainisha kuwa Halmashauri ya Jiji la Mwanza na watekelezaji wa mradi huo, walitia saini mkataba wa makubaliano kwamba baada ya kukamilika kwa machinjio, Halmashauri ya Jiji la Mwanza itaweka mashine za kuchinjia ili machinjio yatumike.

"Timu yangu ya ukaguzi ilifanya ziara tarehe 24 Desemba 2018 na kubaini kwamba machinjio yamekamilika na kukabidhiwa Halmashauri ya Jiji la Mwanza tarehe 15 Agosti, 2018 kwa barua yenye kumbukumbu Namba. LVEMPII/CWMCAIB/VOL.I/73, lakini machinjio hayo hayajaanza kutumika," CAG Assad anabainisha katika ripoti hiyo.

Anaongeza kuwa Halmashauri ya Jiji la Mwanza haijafunga mashine za kuchinjia, jenereta la kutumia gesi na vifaa vingine muhimu vya umeme na pia eneo la machinjio hayo halijawekwa uzio kwa ajili ya usalama.



Rais John Magufuli, akizungumza jambo na Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi (Sugu), baada ya kuhutubia katika eneo la Mafiati, alipowasili jijini Mbeya kuanza ziara ya kikazi. **PICHA: IKULU**

# Serikali yatoa maagizo mazito

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imeelekeza mamlaka zote na wananchi wote wa mikoa ya Lindi, Mtwara na mikoa ya jirani kuchukua hatua za tahadhari ikiwamo kuwahamasisha wananchi wanaoishi kando ya Bahari ya Hindi ili kujiepusha na baa linaloweza kutokea.

Vilevile, imeagiza shughuli zinazofanywa kando na ndani ya Bahari ya Hindi, hususan shughuli ndogo ndogo za uvuvi na usafirishaji wa anga na majini, kusimama.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye

INAENDELEA UK. 8




# Watumishi 190,000 kupandishwa vyeo

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SERIKALI imesema itawapandisha vyeo watumishi 193,166 ambao wamekasimiwa katika ikama na bajeti ya mishahara kuanzia Mei Mosi, mwaka huu.

Mpango huo ulitangazwa jana bungeni jijini Dodoma na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kapteni Mstaafu George Mkuchika, alipowasilisha kauli ya waziri.

"Katika kutekeleza zoezi hili, waajiri wanaelekezwa kwamba kipaumbele cha kwanza kitolewe kwa watumishi wenye utendaji mzuri ambao wanatarajiwa kustaafu hivi karibuni ili waweze kushughulikiwa mapema iwezekanavyo kabla ya kustaafu.

"Kipaumbee cha pili kitolewe kwa watumishi wenye utendaji mzuri waliokaa kwenye vyeo walivyonavyo sasa kwa muda usiopungua miaka minne na kukasimiwa kwenye ikama na bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18," alisema.

Waziri huyo aliwataka waajiri wote nchini kuhakikisha kwamba wanaendesha upandishaji vyeo watumishi stahiki kwa wakati na kwa kuzingatia tange ya taasisi husika, sifa za kimuundo, kuwapo kwa nafasi iliyoidhinishwa katika ikama na utendaji mzuri kwa mujibu wa matokeo ya tathimini ya utendaji kazi (Opras).

Kwa mujibu wa Waziri Mkuchika, waajiri na maofisa wanatakaotekeleza zoezi hilo kinyume cha maelekezo yaliyotolewa na serikali kuhusu upandishaji wa vyeo, watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

"Kama itakavyokumbukwa, zoezi la upandishaji wa vyeo watumishi waliokasimiwa katika ikama na bajeti ya mishahara ya mwaka wa fedha 2015/16 liliahirishwa mwezi Mei 2016 ili kupisha mazoezi ya uhakiki wa watumishi hewa na mishahara batili pamoja na vyeti vya watumishi wa umma.

"Baada ya kukamilika kwa mazoezi tajwa, Rais John Magufuli aliridhia upandishaji vyeo watumishi kwa awamu. Awamu ya kwanza iliyoanzia Novemba Mosi, 2017, ilihusisha upandishaji na uidhinishaji wa taarifa za watumishi 59,967 ambao taarifa zao za kupandishwa vyeo zilikuwamo kwenye mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara (HCMIS), lakini zilikuwa hazijaidhinishwa wakati wa usitishaji tajwa hapo Mei, 2016.

"Awamu hiyo ya pili iliyoanza Aprili Mosi, mwaka jana, ilihusisha watumishi zaidi ya 53,553 ambao walipandishwa vyeo lakini taarifa zao zilikuwa hazijaingizwa kwenye mfumo wakati wa zuio tajwa.

"Uidhinishaji wa taarifa za watumishi 113,520 kwenye makundi haya mawili kupitia mfumo wa HCMIS umekamilika," Mkuchika alisema.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Elimu, Sayansi na Tekenolojia, Prof. Joyce Ndalichako akisalimiana na Balozi wa China Nchini Tanzania, Wang Ke baada ya kumaliza kuhutubia katika hafla ya Maadhimisho ya miaka 55 ya uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na China, iliyofanyika katika Maktaba mpya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam juzi. **PICHA: MAELEZO**

# IGP nchi 7 wakutana Dar uhalifu mipakani

**Na Romana Mallya**

WAKUU wa majeshi la polisi kutoka nchi saba za Afrika Mashariki (EAC), wamekutana kujadili uhalifu unaovuka mipaka na wamesema kuwa matukio ya ugaidi hayana nafasi kwenye umoja wao.

Kikao hicho cha siku mbili ambacho kilifanyika jijini Dar es Salaam, wakuu hao wa majeshi ya polisi wameandaa nyaraka ya makubaliano ya ushirikiano wa pamoja ambayo utaondoa mipaka ya kipolisi na kuruhusu kukabiliana na matukio ya aina zote.

Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, aliwaambia waandishi wa habari kuwa kikao hicho cha siku mbili kimekutanisha wakuu wa nchi kutoka Burundi, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC) na wawakilishi wa viongozi wao wa Jeshi la Polisi kutoka Msumbiji, Kenya, Rwanda, na Uganda.

"Tusiposhirikiana kwa uhalifu wa kuvuka

INAENDELEA UK. 8

# Majaliwa awaelekeza ma-DC, RC vitambulisho wamachinga

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameagiza wakuu wote wa mikoa na wilaya nchini kutotumia nguvu au kulazimisha au kuwapa wajasiriamali wakubwa wenye mapato ya zaidi ya Sh. milioni 4 vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo, kwa sababu hali hiyo inaondoa maana ya uwapo wa vitambulisho hivyo vilivyotolewa na Rais John Magufuli.

"Sasa vitambulisho vile vilivyotolewa kwa wakuu wa wilaya, natambua kwamba maeneo mengine utekelezaji wake sio mzuri kwa sababu wako wengine wanalazimisha watu, badala ya kuwaelimisha namna ya kupata vitambulisho hivyo," alisema Majaliwa.

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mbozi (Chadema), Paschal Haonga, wakati wa maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu.

Akitoa maelezo kuhusu vitambulisho hivyo, Waziri Mkuu alisema yapo maeneo wapo hata wajasirimali wakubwa wenye pato la zaidi ya Sh. milioni 4 ambalo linawafanya

INAENDELEA UK. 8

# Spika Ndugai amvaa Zitto

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe (ACT Wazalendo), anang'anga'nia kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kinyemela.

Kiongozi huyo wa chombo hicho cha kutunga sheria alitoa kauli hiyo bungeni jijini Dodoma jana mchana kabla ya kuahirisha shughuli za Bunge baada ya wabunge kuchangia hoja ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka ujao wa fedha.

"Kusambaza (taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali-CAG) kama anavyofanya Zitto, wakati hii kitu inapaswa ichambuliwe, kama kiongozi lazima uwe na uvumilivu, kazi hiyo ina wenyewe. Anachong'ang'ania Zitto ni kutaka kuwa Mwenyekiti wa PAC kinyemela," Ndugai alisema

Aliongeza kuwa walioko nje ya Bunge hawaelewi taratibu za chombo hicho, akifafanua kuwa kwa kawaida taarifa za CAG zikishawekwa mezani, huwa zinapelekwa kwenye kamati zake ni mbili za PAC na LAAC.

Spika Ndugai alisema kamati hizo huchambua kila kitu, hoja kwa hoja, lakini "watu wanataka kuwaaminisha Watanzania kuwa kila kinachoandikwa na CAG ni kweli asilimia 100".

"Si hivyo tu, yapo mambo kule (kwenye ripoti ya CAG) si kweli hata kidogo, yapo mengi, mengine kiambatanisho hakikuwekwa, mifano ipo mingi, 'book' (kitabu) lile linachambuliwa zinabaki sijui hoja ngapi, ndizo zinapewa serikali kwamba jamani hizi zimalizieni, mengine yote yamefungwa, sijui kiambatanisho hiki hakikuonekana sasa kimeonekana, sijui vocha ile haijaonekana, imeonekana.

"Kwanini (Zitto) anatangulia mbele, oooh! CAG kasema, hiyo ni tuhuma, weka mbele neno tuhuma maana anataka kuwafanya wananchi waamini kuna mahela sijui kuna madudu gani.

"Halmashauri yake ya Kigoma ina hati chafu mwaka wa pili iko kwenye ripoti mle hasemi, na yenyewe itaitwa, itapewa haki ya kusikilizwa, ndiyo maana wabunge wengi wamenyamaza, siyo kama hawajui kusoma yale 'ma-book' kwa sababu ile kazi ina mchakato wake na mwisho tutaelewa nini kilicho ndani."

Alisema haitakuwa haki kwa taifa kama kila kitu kinachoandikwa na ofisi ya CAG kionekane kiko sahihi kwa kuwa ni lazima mtu aliyetiliwa shaka, apewe haki ya kujibu.

"CAG ni 'external auditor (mkaguzi wa

INAENDELEA UK. 8


MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA

TFDA

Tanzania Food & Drugs Authority

MAADHIMISHO YA MIAKA 55 YA MUUNGANO



Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein,
Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Menejimenti na Wafanyakazi wa **Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)** wanaungana na watanzania wote kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli** na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar **Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein**, katika kuadhimisha miaka **55** ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

TFDA inalinda afya ya jamii kwa kuhakikisha ubora, usalama na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA),
Mtaa wa Mwanza, Block T,
Kiwanja Na. 6 S. L. P. 1253,
DODOMA, TANZANIA

*TFDA – Hulinda Afya ya Jamii*

215195902

# Utafiti: Maambukizi malaria yamepungua kwa asilimia 50

**Na Salome Kitomari**

MATOKEO ya utafiti wa viashiria vya malaria katika jamii kwa mwaka 2017 umeonyesha kupungua kwa kiwango cha maambukizi ya ugonjwa huo kwa asilimia 50.

Katika hotuba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ya siku ya malaria duniani, iliyopatikana jijini Dar es Salaam, alisema upungufu huo ni kutoka asilimia 14.8 mwaka 2015 hadi asilimia 7.3 mwaka 2017.

Aidha, utafiti huo umeonyesha kuwapo kwa utofauti mkubwa wa viwango vya maambukizi ya malaria kati ya ukanda mmoja hadi mwingine. Mwalimu alisema kiwango kikubwa cha maambukizi kilikuwa asilimia 24.4 katika Ukanda wa Magharibi mkoani Kigoma, asilimia 15 katika ukanda wa ziwa na ukanda wa kusini.

Kwa mujibu wa Waziri huyo, Ukanda wa Kaskazini ni asilimia moja na baadhi ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini hususan mikoa ya Songwe na Njombe.

"Kutokana na kuboreshwa kwa huduma za afya hususani katika upimaji wa malaria, idadi ya wagonjwa wanaopimwa kwa kutumia kipimo cha MRDT na hadubini na kutolewa kwa taarifa katika mfumo wa utoaji takwimu za Afya (Mtuha) imeongezeka kutoka 16,290 mwaka 2014 hadi milioni 22 mwaka 2018," alibainisha.

Alisema idadi ya wagonjwa wanaothibitishwa kuwa na malaria imeendelea kupungua kutoka asilimia 7.4 mwaka 2014 hadi asilimia 6.2 mwaka 2018.

Waziri Mwalimu alisema wizara kwa kushirikiana na Tamisemi wanatekeleza mikakati ya kupambana na ugonjwa wa malaria kwa kuongeza kinga dhidi ya malaria. "Tunahakikisha kila mwananchi anajikinga na malaria kwa kutumia nyandarua vinavyogawanywa bure, kwa mwaka 2018 hadi sasa vimeganywa vyandarua 6,553,764 kupitia mpango wa chandarua kliniki, kwa wajawazito na watoto chini ya mwaka mmoja kupata wakati wa chanjo ya surua," alisema.

Aidha, jitihada nyingine ni afua ya kuangamiza viluwiluwi vya mbu katika mazalia kwa mwaka 2019 na kwa kushirikiana na Bohari Kuu ya Dawa zimenunuliwa lita 60,000 za viuadudu, pampu 1,000 na vifaa muhmu kama buti ngumu, kofia na overoli zilizosambazwa katika halmashauri 37 za mikoa mitano yenye maambukiza makubwa.

Maadhimisho hayo kitaifa yamefanyika mkoani Lindi na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Air Wing, Kapteni Abel Kilahunja, akisoma historia ya shule hiyo katika mahafali ya kidato cha sita yaliyofanyika shuleni hapo, Ukonga jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Serikali, sekta binafsi kujenga viwanda pamoja

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WIZARA ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Sekta Binafsi zimeingia makubaliano ya uwekezaji wa kujenga viwanda ambavyo vinatumia malighafi ya mabaki ya mazao ya misitu yatakayotumiwa kutengeneza samani kwa matumizi ya taasisi za serikali na majumbani.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Adolf Mkenda, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mipango mkakati ya kikundi kazi cha misitu katika kikao kazi chake mjini Morogoro.

Kikundi kazi hicho cha misitu ni sehemu ya vikundi kazi mbalimbali vya Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), linalounganisha sekta ya umma na sekta binafsi nchini.

Prof. Mkenda ambaye ni Mwenyekiti Mwenza Kikundi kazi hicho kutoka Taasisi ya Umma, alisema jukumu kubwa ni kujadili kwa pamoja na wajumbe wa sekta binafsi kuhusu namna ya kupambana na changamoto mbalimbali ili kuiwezesha sekta ya misitu ikue zaidi.

Alisema miongoni mwa mambo yaliyofikiwa ni namna ya kuhumiza wadau kuongeza na kujenga viwanda ambavyo vinatumia mabaki ya miti kama pumba ili kutengeneza mbao laini zitakazotumika kwa uzalishaji wa samani, hivyo kuongeza ajira, mapato ya serikali na wenye viwanda.

"Tunataka bidhaa zitakazalishwe, soko lianze katika ofisi za Serikali kwa kuwa imezuia uagizaji samani za nje kwa matumizi ya ofisi zake, hiyo ni fursa kubwa kwa viwanda hivi," alisema Prof. Mkenda.

Alisema, Serikali inafanya jitihada kuwahimiza wananchi watambue wajibu wao wa kutunza na kulinda misitu, ambapo mkakati umeandaliwa wa uhimizaji ujenzi wa viwanda vidogo vya asali na uwekezaji wa asali kwa kutumia misitu iliyopo.

Kiongozi mkuu wa Sekta binafsi ya Tasnia ya Misitu na viwanda vya misitu, Ben Mfungo Sulus, alisema bado vipo vikwazo kadhaa havijatatuliwa ikiwamo vya ujenzi wa ujuzi kwa vijana wa namna ya kutumia teknolojia ya kisasa ya mashine za viwandani.

Sulus ambaye pia ni Rais wa Shirikisho la Viwanda vya Misitu Tanzania (SHIVIMITA), aliwashauri watafiti wa mbegu za miti kuzalisha miche ya miti yenye uwezo wa kukua na kukomaa kuanzia miaka minne tofauti na inayochukua miaka mingi. "Ikipatikana mbegu ya aina hii itatoa chachu kwa watu wengi kuchangamkia kilimo cha biashara ya miti, hivyo kuondokana na umaskini wa kipato na pia kuongeza malighafi ya viwanda vya mbao," alisema Sulus.

Naye Kaimu Katibu Mtendaji wa (TNBC), Oliva Vegulla, alisema kuna fursa kubwa katika sekta ya misitu kwa kutoa ajira nyingi zaidi na kuvutia uwekezaji .

# TIC yaitupia lawama TRA kuwafungia wawekezaji

**Na Romana Mallya**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimelalamikia kitendo cha maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kufunga biashara za wawekezaji kinachoathiri juhudi za serikali kuhamasisha uwekezaji nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Geoffrey Mwambe aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam na kueleza kuwa kitendo hicho cha TRA kuwafungia wafanyabiashara na viwanda kwa sababu ya kodi au vibali vingine kwa wawekezaji, kinafufisha hamasa ya uwekezaji.

Mwambe alishauri kuwa hatua ya kufungia biashara au viwanda ingekuwa ni hatua ya mwisho badala ya inavyofanyika sasa.

"Taasisi nyingine zifahamu kuwa kufunga biashara za watu au kiwanda ni kuongeza hasara na iwapo kuna ulazima wa kufunga basi iwe hatua ya mwisho, zipo njia nyingi za kufanya na biashara zikaendelea badala ya kuifunga," alisema.

Alisema kitendo kinachofanywa na maofisa hao ni kwamba hawatapata kodi na biashara hazitakuwepo na mwisho wa siku watakwamisha juhudi za kuhamasisha uwekezaji.

"Mimi ni mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya TRA na katika vikao vya bodi tumekuwa tukijadili namna bora ya kudai kodi na tumekuwa tukikataa kufungia biashara na akaunti za wafanyabiashara," alisema.

Alisema Kamishna Mkuu wa TRA mara kadhaa amekuwa akieleza kufunga akaunti ni mchakato mgumu na siyo kazi rahisi na pale ambapo kutakuwa na kesi maalum zipo taratibu za kufuatwa.

"Lipo wimbi la watumishi wa TRA kwenda kufunga biashara za watu jambo ambalo siyo sawa, ninaumia sana ninapoona yale ambayo tunayazungumza kwenye bodi hayapo kwa watumishi wengine," alisema.

Katika hatua nyingine, Mwambe alimshumkuru Rais John Magufuli kwa namna ambavyo amekuwa akikipigania kituo hicho kufanikisha majukumu yake huku kikitoa.

Alisema Rais Magufuli akiwa ziarani Lindi, Mtwara, Ruvuma na Njombe alitoa maagizo na maelekezo kwa TIC na taasisi nyingine zinazohusika na uwekezaji.

"Huu ni wakati wa kuacha kufikiria misaada na badala yake ni kuweka mipango kufanya uwekezaji, Rais anataka rasilimali zetu zitumike kuleta maendeleo," alisema.

HABARI KITAIFA

# JPM ampa Prof. Mbarawa mwezi kumaliza kero maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

RAIS John Magufuli, amempa mwezi mmoja Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Prof. Makame Mbarawa, kuhakikisha anatatua changamoto ya maji inayowakabili wananchi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya inayowakabili kwa muda mrefu.

Alitoa agizo hilo jana alipokuwa anazungumza na wananchi wa Mji huo baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe akitokea Malawi ambako alifanya ziara ya kikazi.

Wananchi wa Mji wa Mbalizi walisimamisha msafara na kueleza kero zinazowakabili ambapo Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya Vijijini, Sadakati Kimath, alisema Mji huo unakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji.

Alisema mtandao wa miundombinu ya maji hauko vizuri, hivyo unawafanya wananchi hao kutopata maji na maeneo machache yanayopata huduma hiyo kutokuwa ya uhakika.

"Changamoto ya mtandao wa maji ndiyo inayotusumbua sana kwa wilaya yetu hasa Mji huu wa Mbalizi, sisi kama chama tunaona ndio changamoto kubwa kwenye Ilani ya chama," alisema Kimath.

Baada ya malalamiko hayo Rais alimtaka Prof. Mbarawa kueleza sababu ya wananchi hao kukosa huduma hiyo kwa muda yeye kama Waziri anavyokusudia kuitatua.

Prof. Mbalawa alisema kwa sasa wananchi hao wanapata maji kutoka katika Jiji la Mbeya, lakini bado hayatoshelezi mahitaji, hivyo kuna mradi ambao wanaendelea kutekeleza ili kumaliza changamoto hiyo.

Prof. Mbalawa alisema mradi huo utakamilika baada ya wiki tatu na unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni tatu mpaka kukamilika kwake na kwamba huo ndio utakuwa suluhisho la shida ya maji katika Mji huo na maeneo jirani.

"Hatutaki kuwatumia makandarasi kujenga mradi huu maana watatuchelewesha, tukitaka kuwatumia hao watakamilisha baada ya miezi miwili, lakini sisi tumeamua kuwatumia hawa mafundi wetu ambao watatumia wiki tatu kukamilisha," alisema Prof. Mbarawa.

Baada ya maelezo hayo, Rais Magufuli aliwataka wananchi hao kuwa wavumilivu wakati mradi huo unatekelezwa na kwamba kutokana na Waziri kuahidi kukamilisha baada ya wiki tatu, yeye anamuongezea wiki moja ili akamilishe baada ya mwezi mmoja.

Alisema ahadi ni deni, hivyo lazima Serikali ikamilishe mradi huo pamoja na ahadi zingine ambazo ziliahidiwa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ili wananchi waendelee kuiamini serikali yao.

"Kwa muda mrefu wananchi wamekuwa wakisikia siasa na ahadi hizi, sasa Waziri amesema wiki tatu, lakini mimi nampa mwezi mmoja ili akamilishe na muendelee kupata huduma ya maji na nitafuatilia sana," alisema Rais Magufuli.

Alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kuhakikisha anafuatilia ahadi hiyo na kuhakikisha wataalamu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (Mbeya- WSSA) wanapatiwa fedha za mradi huo na kuanza kufanya kazi ndani ya mwezi mmoja.

Alisema ataendelea kufuatilia utekelezaji wa ahadi hiyo kwa Waziri Mbarawa na Waziri anatakiwa kuendelea kufuatilia kwa Mkuu wa Mkoa ili itekelezwe haraka.

Aidha aliwapa pole wananchi wa Mji Mdogo wa Mbalizi kwa matukio ya ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara katika mteremko wa Mlima Mbalizi na kugharimu maisha ya wananchi ambapo aliahidi kupanua barabara hiyo ya Tanzania na Zambia (Tanzam) ili kupunguza matukio ya ajali hizo.

Rais Magufuli alianza ziara ya siku nane katika Mkoa wa Mbeya ambapo ameahidi kutembelea wilaya zote tano za Mkoa huo na Halmashauri zote saba na pia akawapongeza wananchi wa Mkoa huo kwa uchapakazi wanaouonyesha.


SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO)

TAARIFA KWA UMMA



SALIMU BORI ALLY D0861

**Uongozi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)** unapenda kuutaarifu Umma kuwa Salimu Bori Ally (pichani) aliyekuwa Mfanyakazi wa kituo cha IRINGA si mwajiriwa wake tena kuanzia tarehe **12.04.2019.**

Hivyo kwa tangazo hili, Shirika halitohusika na makubaliano yoyote ya kikazi au ya aina nyingine yoyote yatakayofanywa na Salimu Bori Ally kwa niaba ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Imetolewana: OFISI YA UHUSIANO
TANESCO MAKAO MAKUU

21597202

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tudumishe Muungano kwa kuleta maendeleo ya wengi

**LEO** Watanzania tunaadhimisha miaka 55 ya Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar, ambao uliundwa kutokana na makubaliano ya waasisi wa taifa hili.

Waasisi hao, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Mzee Abeid Amani Karume waliamua kuunganisha nchi hizi kwa kutanguliza mbele maslahi ya uafrika; ya kuwaunganisha Waafrika.

Kipindi hicho lilishaanza vuguvugu la kupigania kuwapo kwa taifa moja la watu weusi duniani. Ndio maana ilifanyika mikutano mbalimbali ikiwamo wa Manchester (Uingereza) pamoja na uliofanyika Acra (Ghana). Watu weusi pamoja na kujitambua na kutaka kujikomboa dhidi ya manyanyaso, ubaguzi vilivyotokana na athari za biashara ya utumwa na ukoloni, walikuwa na lengo la kutaka kuwa na taifa lao moja.

Kutokana na kitendo cha waasisi hao kukubali kuunganisha nchi zao na kukubali kila taifa kupoteza baadhi ya maslahi yake, ni jambo la kuwapongeza na kuwaenzi kwa kuwa leo hii matunda ya Uhuru walioupigania yanawanufaisha Watanzania wote. Siri kama taifa moja la Jamhuri ya Muungano tunapaswa kujipongeza kutokana na muungano wetu kudumu kwa muda mrefu. Tunasema hivyo kwa kuwa miaka 55 ni mingi kwa taifa lililoungana kudumu ilikiwa katika umoja na utulivu mkubwa kama ilivyo kwa Tanzania.

Mataifa kadhaa ya Afrika yaliungana miaka michache baada ya Uhuru, lakini muungano wao ulisambaratika baada ya kipindi kifupi. Hatuna nia ya kuzitaja nchi ambazo muungano wao ulisambaratika, lakini kikubwa tunachoweza kusema ni kuwa hapakuwapo na nia ya dhati ya kuungana.

Nchi zinazoungana kwanza zinapaswa kuwa na maslahi yanayofanana na wananchi wake ni lazima wawe wamekubali kwa hiyari yao. Muungano ambao ni wa maslahi ya viongozi hauwezi kudumu daima kwa sababu huko mbele wananchi wataukataa watakapoona hawana maslahi hao. Kimsingi hichi ndicho kilichotokea kwa mataifa ambayo muungano wao ulisambaratika.

Tunawapongeza Watanzania kwa kudumisha muungano wetu kwa kipindi chote cha miaka 55 ambao ni umri wa mtu mzima bila kuwapo na mawimbi makubwa ya kuuyumbisha.

Siri ya muungano wetu kuendelea kuwa imara ni kutokana wa wananchi wa pande zote kupendana na kuheshimiana, mambo ambayo yamewawezesha kuwa ndugu. Pia tunazipongeza serikali zote mbili mara kwa mara kutumia njia za majadiliano pale zinapojitokeza changamoto.

Tunaiona njia hiyo kuwa ndiyo itakayowezesha muungano wetu kuendelea kuwa imara kwa miaka mingi ijayo na kuwa mfano kwa mataifa mengine Afrika na duniani.

Hata hivyo, tunaona kuwa kuna haja ya kuchukuliwa hatua kwa njia ya vitendo zaidi za kuyaboresha zaidi mambo ambayo waasisi wetu waliyaamini, kuyaanzishana kuyasimamia kwa dhati. Kimsingi Mwalimu Nyerere na Mzee Karume waliokuwa na falsafa inayofanana ya kuwaletea maendeleo watu wote, hivyo kujikita katika mapambano dhidi ya umaskini, ujinga na maradhi.

Kwa bahati nzuri viongozi wetu waliopita na waliopo wameendeleza jitihada hizi, hivyo tunashauri kwamba ziendelee kwa kasi lengo likiwa kuondoa matabaka na kuwawezesha wanyonge kunufaika na matunda ya uhuru pamoja na mapinduzi ya Zanzibar.

Jitihada za kupambana na rushwa na ufisadi zinazotekelezwa na serikali zote mbili za sasa ni ishara kuwa viongozi wetu Rais John Magufuli na Dk. Ali Mohamed Shein, wanataka kila mwananchi apate maendeleo na kunufaika na rasilimali za taifa. Watanzania wote tuwaunge mkono ili kila mmoja anufaike na kupata maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Jamani, kutoka 'heroine' hadi sumu ya panya?

**MAMLAKA** ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, ilishatangaza kuongeza nguvu zaidi kupambana na wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya, ili kuokoa nguvukazi ya taifa. Ni mkakati wa kutokomeza mtandao huo.

Kamishna Mkuu wa mamlaka hiyo, Rogers Sianga, alikaririwa akisema serikali inataka kutokomeza mtandao wote wa wanaojihusisha na biashara hiyo, ili kuokoa kizazi kilichopo na kijacho.

"Dawa za kulevya zinaathiri sana nguvu kazi ya taifa na tangu mamlaka hii imeanza tumefanikiwa kudhibiti uingizaji wa Heroine, Cocaine na dawa nyingine za kulevya na tumewakamata wafanyabiashara wakubwa waliokuwa wanatafutwa na mataifa makubwa na hiyo ni hatua kubwa kwa nchi yetu katika mapambano haya," alikaririwa na vyombo vya habari akisema.

Aidha, akasema serikali imepanga kuongeza vituo vya kuhudumia waathirika wa dawa za kulevya katika mikoa ya Mbeya, Dodoma na Mwanza kwa awamu ya kwanza kutokana na mafanikio yaliyofikiwa katika kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya na matumizi yake.

**Aidha, akasema serikali imepanga kuongeza vituo vya kuhudumia waathirika wa dawa za kulevya katika mikoa ya Mbeya, Dodoma na Mwanza kwa awamu ya kwanza kutokana na mafanikio yaliyofikiwa katika kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya na matumizi yake.**

Pamoja na juhudi hizo, watumiaji wa dawa hizo wanadaiwa kuibuka na mbinu nyingine za kuendeleza matumizi hayo.

Inaelezwa kuna baadhi ya vijana nchini wanaotumia sumu ya kuua panya kama dawa ya kulevya. Hiyo ni baada ya dawa walizozoea kuadimika, kutokana na vita kubwa kutoka serikalini.

Hivi karibuni imeripotiwa 'mateja' nchini sasa wanachanganya sumu ya panya na dawa nyingine za kulevya, ikiwamo bhangi na kisha wanavuta, ili kufanikisha kinachoitwa 'kukata kiu.'

Inaelezwa hiyo ni hatari zaidi ya dawa za kulevya zilizozoeleka kama Coccaine na Heroine. Ni mwelekeo wa madhara makubwa zaidi.

Vijana wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 35 ndio wanaodaiwa kujihusisha na matumizi ya dawa hizo na kudidimiza zaidi nguvukazi ya taifa na wanaishia kuwa mzigo kwa familia, jamii na taifa.

Vita dhidi ya dawa hizo ilitosha kuwa fundisho kwao kwa kuachana kabisa na biashara hiyo siyo kubuni njia nyingine kama hiyo ya kuchukua sumu ya panya na kuchanganya na bangi.

Athari ni kwa mishipa ya damu ya ubongo inasinyaa na kusababisha kupata kiharusi, hata kwa kijana. Vilevile, mtu anaweza kupata ugonjwa wa akili.

Aidha, kwa upande wa moyo ni inaleta shinikizo la damu, pia mapigo ya moyo yasiyo kawaida, ikiishia mtu kufa ghafla.

Kuna madhara mengi yanayoelezwa kusababishwa na dawa za kulevya, lakini inaonekana kuna watu wanaokuwa wagumu kubadilika, hadi kufikia kubuni mbinu mbadala wa sumu ya panya.

Watu hao wanatafuta nini hasa? Ni vyema wakafanya 'maamuzi magumu' ya kujitenga na dawa hizo, haraka ili kunusuru maisha yao kwa kwenda kwenye vituo maalum vilivyoandaliwa kwa ajili yao.

Pia, sisi tunaowazunguka, vivyo hivyo hata kama ni ndugu zetu tuwachukulie 'maamuzi magumu' kuwanusuru

MJADALA

# Kwa hatari hii, inakuwaje miwani iendelee kiholela?

Na Lazaro Mateko

MAZOEA ya baadhi ya Watanzania kupenda kununua miwani mitaani na kuvaa, yaelezwa kuwa ni kukaribisha upofu, iwapo hawataachana nayo na kufuata malekezo ya madaktari wa macho.

Mwani ya urembo maarufu kama ile 'ya jua' inatajwa kuwa na madhara kwa watumiaji wake, kutokana na watu hawafahamu saizi au namba wanazopaswa kuvaa, kabla ya kuinunua.


Baadhi ya madaktari wanakemea uvaaji huo na kuwataka wazingatie maelekezo sahihi. Hata hivyo, inaonekana elimu hiyo haijazaa matunda ya kutosha, kwani uvaaji unaendelea katika sura ya urembo.

Miaka kadhaa iliyopita, bingwa wa upasuaji wa macho, kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Dk. Neema Kanyaro, alihojiwa na redio moja akikemea uvaaji huo na madhara yake.

"Miwani ni dawa, lakini usivae bila kupima, kwani inaweza kukusababishia matatizo ikiwamo uoni hafifu. Unaweza kukuta unavaa miwani myeusi lakini kumbe siyo namba yako. Kama hujijui unaweza kukuta ukitazama unaona giza kumbe umeshaua macho kwa urembo," anasema Dk. Kanyaro.

Anasema kila tatizo la macho lina hatua zake, hivyo halina budi kufanyiwa marekebisho, kwa miwani inayolingana na hali halisi ya kiwango cha kasoro ya uono kwa wakati huo.

Anasema uvaaji miwani ya jua kama urembo bila ya kwenda kupima kujua na aina gani ya miwani wanayotakiwa kutumia, pasipo kujua namba yake kutokana na uono wake.




Hivi karibuni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, naye alikemea uvaaji miwani kiholela, akikumbUsha jamii kuwa jicho ni kiungo muhimu cha mwili wa mwanadamu na akatahadharisha uvaaji wa miwani ya urembo.

Anasema takwimu zinaonyesha, katika kila watu 100, wanne kati yao wanakabiliwa na ubovu wa macho, na kwamba idadi inaweza kuongezeka, iwapo wananchi hawatakuchukua hatua za kujikinga.

Waziri Ummy, alikuwa akizindua kambi ya kutibu macho iliyoandaliwa na asasi ya Maendeleo ya Wanawake Mkoa wa Tanga (Tawode) na akafafanua kuwa katika watu hao wanne, mmoja kati yao hubainika kuwa na upofu na wengine watatu wanasumbuliwa na uoni hafifu.

Anasema, mbali na kuvaa miwani bila kupima, anataja sababu nyingine zinazochangia kuharibika kwa macho kuwa ni watu kula vyakula visivyo na Vitamini 'A' pia, kula kwa 'mawazo' mboga za majani na matunda.

Kwa upande wa miwani ya urembo, ni kwamba inapatokana kwa wingi mitaani na inauzwa kienyeji, watu wengi wakichangamkia na kuivaa kama urembo au kupunguza makali ya miale ya jua, nayo tatizo. Wapo wanaoivaa ili watu wasiwatambue kirahisi, lakini jambo la msingi hapa ni kwamba siyo vizuri kuvaa miwani bila maelekezo ya wataalam wa afya, mwisho unaweza kuwa mbaya.

Tahadhari zimeshatolewa na zinaendelea kutolewa. Hivyo, ni wajibu wa jamii kuzingatia, ili kulinda afya ya macho, kuliko kuendekeza urembo na mwisho wa siku, yakaharibika.

Waziri Ummy anakumbusha kuwa, jicho ni kiungo muhimu cha mwili wa mwanadamu na anatahadharisha juu ya uvaaji wa miwani ya urembo, akitambua kuwa siyo sahihi kuivaa bila maelekezo ya daktari.

Hivi sasa mitaani ni jambo la kawaida, kukuta wazazi na walezi wakiwanunulia watoto wao miwani hiyo.Watu waliozoea mtindo huo, ni vyema wakatambua kuwa wanawaumiza watoto, kwa sababu uvaaji huo siyo salama.

Iwapo watashindwa kubadilika, basi ni bora uuzwaji wa miwani hiyo kiholela ukapigwa marufuku, ili kunusuru afya za Watanzania, Ni bora kupata matatizo ya macho kwa bahati mbaya, lakini siyo kwa kupenda.

Uuzwaji miwani hiyo kiholela ukiachwa uendelee, unaweza kusababisha Watanzania wengi, wakiwamo watoto na vijana kuishia katika uoni hafifu, kabla ya kufikia umri wa utu uzima.

Miwani ni miongoni mwa maadui wa macho, kama haitumiwi vizuri, Kila mtu hana budi kuzingatia, kile ambacho wataalam wa afya wanasisitiza, vinginevyo madhara ni makubwa.


**Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-**

- **Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=**
- **Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=**
- **Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima**
- **Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku**



# IGP nchi 7 wakutana Dar uhalifu mipakani

INATOKA UK. 3

mipaka hatuwezi kufanikiwa kwa sababu wahalifu wanashirikiana wanakaa wanapanga, kwa ushirikiano huu tunawaambia wahalifu wa aina zote hasa magaidi kuwa hawana nafasi kwenye nchi hizi," alisema.

IGP Sirro alisema watajadili kuhusu uhalifu wa usafirishaji wa binadamu ugaidi, uhalifu wa kimtandao pamoja na aina nyingine ya na uhalifu unaovuka mipaka.

"Wahalifu wana tabia ya kuvuka mipaka kutoka nchi moja kwenda nyingine lazima kama majeshi tuwe na mikakati madhubuti ya kukabiliana nao, baada ya kikao hiki mhalifu atakayefanya uhalifu nchi moja na kukimbilia nchi nyingine hata kuwa na nafasi, tutawadhibiti," alisema.

Alisema ushirikiano huo wa nchi hizo saba ni wa kudumu na utawafichua wahalifu kwenye maficho kwa sababu Jeshi la Polisi litakuwa halina mipaka katika kazi zao.

Mkuu wa Jeshi la Polisi DRC, Dieudonne Amuli Bahigwa, alisema nchi yake mara kwa mara imekuwa ikisumbuliwa na wahalifu ambao mara baada ya uhalifu wao hukimbilia nchi za jirani kujificha.

"Kikundi cha waasi ADF kinashirikiana na vikundi vingine kutoka ndani na nje ya nchi ili kutekeleza uhalifu wao Congo, tunaamini mkutano huu utawezesha nchi hizi kuwa na ushirikiano wa kupambana na wahalifu wa aina hii badala ya nchi moja kufanya hivyo," alisema.

Alisema nchi yake imeshirikiana na mataifa mengine na kupambana nao, hatua iliyosaidia kwa kiwango kikubwa kuwadhibiti waasi hao.

Mkuu wa Jeshi la Polisi Rwanda, Dan Munyuza, alisema kupitia mkutano huo wakuu wa jeshi la polisi watatoka na lengo moja la kuhakikisha nchi zao zinapambana na uhalifu wa kuvuka mipaka na kupitia intelijensia zao zitasaidia kubaini maficho ya wahalifu na kuwadhibiti.

Naye, mwakilishi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi Kenya, Julius Kanmpiu, alisema tukio la kigaidi lililotokea mwanzoni mwa mwaka huu kwenye hoteli ya kifahari ya DusitD2 linaweza kutoka mahali popote katika nchi yoyote na wakati wowote.

"Milipuko iliyotokea DusitD2 inaweza kutokea mahali popote, nchi yoyote na wakati wowote, ili kuhakikisha tunadhibiti tunapaswa kuwa na ushirikiano wa pamoja kwa kuitekeleza kwa vitendo mikakati tulijiwekea," alisema.

Kanmpiu alisema mpaka sasa nchi hiyo imeweza kupambana kwa kiwango kikubwa na uhalifu wa kigaidi na wa aina nyingine kwa kushirikiana na wadau kutoka nchi mbalimbali.

Naye, Mwakilishi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi Uganda, Byakagaba Abas, alisema nchi yake imekuwa ikishirikiana na za EAC na wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuhakikisha wahalifu wanachukuliwa hatua za kisheria wanapobainika.

# Spika Ndugai amvaa Zitto Kabwe

INATOKA UK. 3

nje), anapotoa hoja lazima hoja zile zitafutiwe majibu. Kama kwenye hoja zile kuna polisi, watapewa polisi washughulike na mtu huyo, kama kuna ya serikali, wanapewa serikali wajue cha kufanya.

"Sasa mwenzetu huyu (Zitto) harakahara ili aonekane yeye kama yeye 'is the best' (ni bora) lakini Bunge na wabunge wote hawajui kusoma taarifa, jambo ambalo si sawa," Spika Ndugai (pichani) alisema. Alisema hawmkatazi Zitto kufanya hivyo kwa kuwa havunji kanuni yoyote, lakini hafurahishwi na "kule kuwahiwahi sijui kunaitwaje, anaonekana wa maana eti ana taarifa, taarifa ziko wazi".

Alisema ni vizuri wabunge wakajua taratibu na namna ya kwenda na watakwenda vizuri katika maisha yao ya kibunge, akiwakumbusha kujizuia kuwatuhumu watu ambako alisema ni dhambi kwa Mungu.

"Wape nafasi hao waliotajwa wajieleze kama wakiwa hawana maelezo, sasa toka nje kaeleze kuna watu wameitwa hawakujieleza, hawakuchukuliwa hatua, itakuwa jambo sahihi lakini taarifa mezani tayari. "Hata yule wa Chadema tunaweza kusema lile gari kumbe si kweli na ataitwa, mimi kazi yangu lazima waitwe, anaitwa kwenye kamati ya PAC na asiyefika nitamleta kwa pingu. Si madaraka mmenipa! Kuna atakayeshindikana kuitwa? hakuna hata mmoja, wajipange!" Spika Ndugai alisisitiza.



Hivi karibuni, kiongozi huyo wa Bunge aliweka wazi kuwa Zitto ni mbunge anayemsumbua, lakini anasita kuchukua hatua dhidi yake kwa kuwa chama chake kina mbunge mmoja, hivyo anaona kitakosa uwakilishi bungeni.

# Serikali yatoa maagizo mazito

INATOKA UK. 2

Ulemavu, Jenista Mhagama, alitangaza maagizo hayo alipotoa kauli ya serikali jana bungeni jijini Dodoma kuhusu Kimbunga cha Keneth.

Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) ilitangaza Jumatatu kuwa kimbunga hicho kilikuwa kilomita 450 kutoka pwani ya Mtwara na kilikuwa na kasi ya kilomita 130 kwa saa.

TMA ilieleza kuwa kimbunga hicho kilitarajiwa kuongeza nguvu zaidi jana mchana kikifikia kilomita 170 kwa saa na kingekuwa kilomita 150 kutoka pwani ya Mtwara.

Akitoa kauli ya serikali kuhusu kimbunga hicho, Waziri Mhagama alisema kufuatia utabiri huo, kuna uwezekano mkubwa kimbunga na mafuriko kutokea katika mikoa ya Mtwara na Lindi na mikoa mingine ya jirani.

"Kwa msingi huo, kunatarajiwa kutokea kimbunga chenye kasi ya kilomita 130 kwa saa katika uelekeo wa mashariki kwa umbali wa kilomita 175 kutoka pwani ya Mtwara, kimbunga hicho kinatarajiwa kuendelea kusogea kuelekea pwani ya kusini ya nchi yetu na kitaambatana na mafuriko kwa sababu mikoa ya Lindi na Mtwara ipo chini ya usawa wa bahari," alisema.

"Hali hiyo inatarajiwa kuleta athari mbalimbali ikiwa ni pamoja na mafuriko na upepo mkali vinavyoweza kupelekea athari na uharibifu wa makazi, mazao shambani, miundombinu kutokana na kuongezeka kwa kina cha maji katika Bahari ya Hindi.

"Shughuli za usafirishaji wa anga na majini zinaweza kuathirika hasa kwa mikoa ya Lindi na Mtwara kutokana na hali mbaya ya hewa inayotabiriwa."

Alisema serikali imeelekeza mamlaka zote na wananchi wote wa mikoa ya Lindi, Mtwara na mikoa ya jirani kuchukua hatua za tahadhari ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wananchi wanaoishi kando ya Bahari ya Hindi.

"Tunaendelea kusisitiza kamati za maafa katika ngazi zote katika maeneo husika kwa mujibu wa sheria tuliyonayo, kufuatilia kwa karibu na kwa kina jambo hili, naendelea kuelekeza uongozi wa ngazi zote kutoka katika mikoa ya Lindi na Mtwara kutoa tahadhari katika mitaa mbalimbali pamoja na hatua mbalimbali za kuchukuliwa," aliagiza.

Alisema serikali imetoa rai kwa taasisi mbalimbali za umma na taasisi binafsi kuendelea kufuatilia na kujiandaa kutoa misaada mbalimbali ya kibinadamu endapo hali hiyo itajitokeza.

Waziri Mhagama ambaye pia ni Mnadhimu wa Shughuli za Serikali Bungeni, alisema pamoja na kazi nzuri inayoendelea kufanyika kwa sasa, serikali inaendelea kuelekeza hatua stahiki zichukuliwe ili kupunguza madhara makubwa ya kimbunga na mafuriko kama yatatokea kama ilivyotabiriwa na TMA.

"Serikali kwa kuzingatia Sheria yetu ya Maafa Na. 7 ya Mwaka 2015 na kanuni za usimamizi wa maafa ya mwaka 2017, inaendelea kusisitiza kamati za maafa kupitia ngazi ya vijiji mpaka wilaya kuhakikisha tunakuwa pamoja na kushirikiana na wananchi katika kuhakikisha tunakabiliana," aliagiza.

Alisema Ofisi ya Waziri Mkuu na hasa idara ya maafa itaendelea kuchukua hatua stahiki kuhakikisha wananchi wanakuwa salama.

### HALI ILIVYO KUSINI

Hamaki ilitanda miongoni mwa wananchi wengi wa mikoa ya Lindi na Mtwara kutokana na

INAENDELEA UK. 26

# Majaliwa awaelekeza ma-DC, RC vitambulisho

INATOKA UK. 3

na wao washindwe kuchangia pato la taifa kulingana na biashara wanazofanya, kwa sababu wao kwa kipengele chao wanachangia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) moja kwa moja.

"Kwa hiyo waheshimiwa wabunge ni kwamba waheshimiwa wakuu wa wilaya na mikoa, (naelekeza) watumie muda wao kuelimisha, nani anapaswa kuwa na kitambulisho badala ya kutumia wakati mwingine nguvu au kwenda kulazimisha au kuwapa wajasiriamali wakubwa wenye mapato ya zaidi ya Sh.milioni 4 na kuondoa maana ya uwapo wa vitambulisho," alieleza Waziri Mkuu.

Alisema serikali imeipokea hoja hiyo na wanaendelea kutoa maelekezo kwa wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya, kutumia nafasi hiyo kuelimisha zaidi kuliko kulazimisha.

Waziri Mkuu aliwaasa wakuu wa mikoa na wilaya watumie nafasi hiyo kuelimisha ni nani anatakiwa apate kitambulisho hicho ili kuwaondolea usumbufu wa kuwa wanatozwa tena Sh. 200 au Sh. 500 kila siku mjasiriamali anapoendelea kufanya kazi yake ya kuuza mchicha, maandazi na wale wanaouza mahindi kwenye mabasi, kwa kuwa hao ndio ambao Rais Magufuli aliwalenga ili na wao waone uchangiaji wa uchumi, pato la nchi ni sehemu yao.

Aidha, alieleza kuwa nia ya serikali ni kuona pia wanaendelea kufanya biashara yao bila kusumbuliwa ndani ya mwaka kwenye halmashauri zao na kwamba serikali imeipokea taarifa hiyo na itaifanyia kazi zaidi ili kuleta utendaji ulio sahihi na wajasirimali waweze kujitoa kuchangia uchumi wao.

Akitoa ufafanuzi zaidi, Waziri Mkuu alisema ni kweli kwamba serikali imeweka utaratibu mzuri sana wa kuwafanya wajasiriamali wadogo waweze kuchangia pato la taifa na Rais Magufuli alibuni njia nzuri sana, ambayo inawatambulisha wajasiriamali hao.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, wajasiriamali hao wamewekwa kwenye madaraja yao, ambapo wapo wadogo, wamo wafanyabiashara wa kati na wajasirimali wakubwa.

Katika swali lake la msingi, Haonga alisema suala la vitambulisho kwa wajasiriamali wadogo wadogo limekuwa ni kero kubwa sana katika maeneo mbalimbali nchini na limekuwa ni kero kubwa kwa wale wajasiriamali wanaouza mboga kama michicha na nyanya, lakini hata wanaouza njegere, maandazi na vitumbua.

Alieleza kibaya zaidi, maeneo mengine hata wale wanaotoka shambani amechuma mchicha wake anaambiwa naye ni mjasiriamali alipe Sh. 20,000 ili apewe kitambulisho.

### USUMBUFU DHIDI YA WAWEKEZAJI

Kuhusu suala la wawekezaji wengi kudaiwa kukwamishwa na kusumbuliwa sana, Waziri Mkuu alisema ili kusimamia uwekezaji kwa ukaribu zaidi, Rais Magufuli aliunda Wizara mpya ya kushghulika uwekezaji ili kusaidiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

"lengo hapa ni kuhakikisha kwamba tunaondoa usumbufu ambao wanaupata wawekezaji hao ili kuweza kuwekeza kwa urahisi zaidi. Hata hivyo kwenye uwekezaji sasa, tumefikia hatua nzuri sana, moja; tumetengeneza andiko maalum (Blue Print) ambayo imeonyesha njia rahisi za uwekezaji hapa nchini kwa lengo la kuondoa usumbufu kwa wawekezaji wetu na kwa hiyo tumetengeneza mazingira rahisi juu ya uwekezaji," alieleza Waziri Mkuu

"Lakini mbili; tumeboresha kituo cha uwekezaji kwa kukaribisha wizara zote zinazoguswa na uwekezaji kwa kuwa na mtu wao pale kwenye taasisi ili mwekezaji anapokuja huduma zote kama alitakiwa kwenda wizara ya ardhi, akitaka kwenda Brela (Mamlaka ya Usajili wa Biashara na Leseni), tuna idara kama 10 au 11 ambazo ziko pale za kumhudumia mwekezaji na baada ya Wizara hiyo kuwa imeletwa Ofisi ya Waziri Mkuu."

# Wanafunzi wawashtaki wazazi wao kuwatuma kutafuta fedha

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WANAFUNZI wamewatuhumu wazazi na walezi wao kuwa wamekuwa wakiwatuma kwenda kutafuta fedha kwa ajili ya kukidhi matumizi ya nyumbani.

Hayo yalibainishwa kwa nyakati tofauti na wanafunzi wa kike katika shule za sekondari za Mataka na Namasakata katika mdahalo wa kujadili hatima ya msingi wa maendeleo ya Vijana ulioandaliwa na Shirika lisilo kuwa na Kiserikali la Youth Development Foundation.

Wanafunzi hao walieleza kuwa kitendo cha wazazi na walezi kuwataka watoto wao kwenda kutafuta fedha kinamaanisha kwamba wanawatuma waende kujiuza hivyo kusababisha wapate matatizo hususan mimba za utotoni.

Walisema kufutia hali hiyo, vitendo hivyo vimekuwa ikiwafanya watoto wao wa kike kupata mimba zisizotarajiwa, na katika umri mdogo. Pia wanafunzi hao walisema kuwapo kwa mafunzo ya kimila ya unyago kwa watoto wa kike na jando kwa watoto kiume wakiwa na umri mdogo, ni miongoni mwa vitendo mbavyo vimekuwa vikichochea watoto hao kwenda kujaribisha kwa matendo ili kujionea uhalisia wa tendo la ndoa ambao hufundishwa katika kipindi hicho.

Aidha, katika taarifa hiyo pia watoto hao walidai kumekuwa na tabia za wanawake wanye umri mkubwa wanaojihusisha na biashara ya ukuwadi na udalali, ambao huwashawishi na hata kuwatafutia wananume wa kwenda kufanya nao vitendo hivyo.

Wakitoa elimu ya kujikinga na mimba za utotoni, Afisa Ustawi wa Jamii wilaya ya Tunduru, Brandina Sekela na msaidizi wake, Farida Kayombo, walisema kuwa mimba nyingi zisizo tarajiwa kwa watoto chini ya miaka 18 zimekuwa zikitokana na watoto hao kuiga tabia za makundi rika, tamaa na kutokuwapo kwa usimamizi thabiti wa malezi kutoka kwa wazazi wao.

Walisema takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2018 jumla ya watoto wa kike 1,538 wenye umri wa kati ya miaka 13 hadi 17 waliripotiwa kupata ujauzito na kujifungulia katika hospitali, vituo vya afya na zahanati zilizopo wilayani Tunduru.



Kaimu Mkurugenzi wa Biashara wa Vodacom Tanzania, Linda Riwa (mbele), akizungumza na wananchi wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Data Datani katika viwanja vya Mbagala Zackiem jijini Dar es Salaama jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makandarasi waiangukia serikali

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Makandarasi Wazalendo Tanzania (ACCT), kimeiomba serikali irudishe imani kwao na kuwapa kazi.

Mwenyekiti wa chama hicho, Milton Nyerere, alitoa ombi hilo jana jijini Dar es Salaam katika mkutano mkuu wa nane wa mwaka.

Nyerere aliiomba serikali iweke nia ya dhati ya kuwainua kiuwezo kwa kuwalazimisha wakandarasi wa kigeni wanapofanya miradi mikubwa kushirikiana na wazawa kwa kuwapa baadhi ya kazi katika miradi hiyo.

Alisema kumekuwapo na hisia miongoni mwa makandarasi hasa wazawa kuwa hawaaminiki tena na serikali.

"Hii inatokana na matamko ya viongozi mbalimbali wa serikali pamoja na uamuzi wa serikali kutoa kandarasi kwa taasisi zilizo chini ya serikali au mashirika ya umma," alisema.

Alisema suala hilo limeunganishwa na ukosefu wa uzalendo, wizi pamoja na rushwa ya kwamba bei za makandarasi wazawa ziko juu.

"Chama kinaiomba serikali kurudisha imani kwa makandarasi maana siyo wote wanaofanya kazi vibaya, kuna wengi ambao wako vizuri na wanafanya vyema kazi zao," alisema.

Aliiomba serikali kuweka nia ya dhati ya kuwasaidia na kuwainua ili waweze kushiriki kikamilifu kuimarisha na kujenga uchumi wa nchi.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Msajili mstaafu wa Bodi ya Makandarasi (CRB), Boniface Muhegi, ambaye alikuwa mgeni rasmi, alieleza kuwa ili makandarasi wawe wakubwa, wanatakiwa kuacha ubinafsi, washirikiane na kampuni zilizopiga hatua kwa kuwa baada ya kumaliza kazi, watabakia na ujuzi.

Alisema mwaka ujao wa fedha utakuwa na kazi nyingi kubwa, hivyo kukishauri chama chao kujipanga ili wanachama wake wawamo katika miradi ya ubia.

"Msisubiri kazi zitangazwe, anzeni kubuni namna ya kutafuta fedha kwa ajili ya miradi, kwa sasa kuna taasisi mbalimbali za kifedha zinazotoa mikopo kwa gharama nafuu, mnakaa na serikali kuangalia namna ya kufanikiwa kwenye hilo," alisema.

Aliwataka watafute ufumbuzi wa matatizo yao kwa kushirikiana na serikali badala ya kila mwaka wanapokutana kuishia kuainisha changamoto.

## Vodacom yadatisha wateja wake

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA wa Vodacom Tanzania wamewezeshwa fursa mpya ya kupata bonasi ya MB baada ya hampuni hiyo ya simu za mkononi kuzindua kampeni ya data iitwayo "Data Datani'. Imeelezwa kuwa kampeni hiyo inawezesha wateja wake kupata bonus Mb hadi mara mbili zaidi kila wanunuapo bando la intaneti. Kampeni hiyo ilizinduliwa jana katika viwanja vya Mbagala Zackhem jijini Dar es Salaam. Kwa mujibu wa kampuni hiyo, Kampeni ya Data datani inalenga kuwawezesha watumiaji wa intanet kufaidi zaidi matumizi ya vifurushi vyao, na pia kuwajuza mbinu mbali mbali za kutunza data isiishe kwa haraka, jambo ambalo limekuwa likiwatatiza wateja wake kwa muda mrefu.

Katika uzinduzi wa kampeni hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Biashara wa Vodacom Tanzania Plc, Linda Riwa, alitilia mkazo umuhimu wa data katika maisha ya kila siku.

"Tukiwa ni Kampuni inayoongoza nchini kwa kutoa intaneti yenye kasi zaidi, ni muhimu kuzingatia pande zote mbili za sarafu, yaani huduma na wateja wetu. Ndio maana tumeleta kampeni hii ili kuwawezesha wateja wetu kupata zaidi ya kile walicholipia kila wanaponunua bando la data," alisema Linda na kuongeza: "Wanafahamu umuhimu wa data hasa katika zama hizi za kidijitali, habari zote na biashara ziko mitandaoni, hivyo wasingependa ukosefu wa data uwe kikwazo kwa wateja wao katika kufanikisha shughuli zao za kila siku."

Mwaka 2017 Kampuni ya Vodacom Tanzania ilizindua mtandao wa 4G katika mkoa wa Dar es Salaam ili kuwawezesha wateja wake kupata intaneti yenye kasi zaidi, na mpaka sasa mtandao wa 4G umesambaa kufikia mikoa 24.

Mfanyabiashara na mkazi wa Mbagala, Mwajuma Hamisi, aliyehudhuria uzinduzi huo alisema: "Sasa ni wakati wa kudata datani, intaneti sio tu teknolojia bali pia ni kiuwezeshaji. Inatuwezesha kupata habari haraka, inatuwezesha kufanya biashara za mtandaoni, inawezesha serikali kupata kipato na kuwezesha shughuli za kijamii, yani kudata, ni zaidi ya data tu."

# 'Fedha lazima itumike uchaguzi serikali mitaa'

BUNGE limeelezwa kuwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unahitaji rasilimali fedha ili kuwezesha upatikanaji wa mahitaji mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi huo.

Gharama zingine ni uendeshaji wa uchaguzi huo ikiwamo mafuta ya magari, matengenezo ya magari na posho mbalimbali kwa ajili ya watu watakaoshughulikia mchakato mzima wa uchaguzi huo.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, aliyasema hayo bungeni jijini Dodoma jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Aida Khenan (Chadema).

Mbunge huyo alihoji sababu za serikali kutenga na kutumia fedha katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vitongoji na vijiji.

Katika majibu yake kwa mbunge huyo, Waitara alisema madhumuni ya kuanzishwa kwa mamlaka za serikali za mitaa kama ilivyotajwa kwenye Ibara ya 146(2)(a)-(c) ya Katiba ni kuimarisha demokrasia na kuitumia demokrasia katika kuharakisha maendeleo.

Alisema katika kutekeleza jukumu hilo muhimu, viongozi wanaoongoza vyombo vya serikali za mitaa huchaguliwa kwa njia ya kidemokrasia kupitia uchaguzi wa serikali za mitaa katika ngazi hizo.

"Uchaguzi wa serikali za mitaa unahitaji rasilimali fedha ili kuwezesha upatikanaji wa mahitaji mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi vikiwamo vifaa vya uchaguzi kama vile masanduku, lakiri na fomu pamoja na gharama zingine mbalimbali za mafuta na posho," alisema.

Waitara alisema zipo taratibu za kisheria ambazo zinapaswa kufuatwa katika uchaguzi huo kama vile kutoa matangazo ya serikali yanayohusu uchaguzi.

Aliongeza kuwa mchakato wa uchaguzi huo huhusisha vikao mbalimbali na wadau wa uchaguzi kuhakiki maeneo au majimbo ya uchaguzi na kuandaa daftari la wapigakura na kuratibu shughuli hizo zote kunahitaji rasilimali fedha.

"Hivyo, ili kukamilisha uchaguzi wa serikali za mitaa ni lazima serikali itenge fedha za kugharamia shughuli za uchaguzi huo kama ilivyo kwa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani," alisema.

Baada ya majibu hayo ya Waitara, Spika wa Bunge, Job Ndugai alisema mwaka huu kimbembe kitakuwapo katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

"Mwaka huu kimbembe uchaguzi wa serikali za mitaa, tutajua nani ni nani," Spika Ndugai alisema.



Daktari wa magonjwa ya moyo kwa watoto kutoka Hospitali Kuu ya Jimbo la Shandong la nchini China, anayejitolea katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Zhao Lijian (kushoto), akiwaelezea madaktari wenzake kutoka China anavyotoa huduma ya matibabu ya moyo kwa watoto walipotembelea taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JKCI**

# Kibali ajira za walimu kutolewa mwezi ujao

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(Tamisemi), inatarajia kupata kibali cha kuajiri walimu ndani ya miezi miwili ijayo, Bunge limeelezwa.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mwita Waitara, akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Felister Bura (CCM).

Mbunge huyo alitaka kujua mkakati wa serikali kuhakikisha inaajiri walimu wa masomo ya sayansi wanaotosheleza mahitaji.

Bura pia alisema kuna uhitaji wa walimu wa shule za msingi kwa Mkoa wa Dodoma.

Akimjibu mbunge huyo, Waitara alisema serikali inatarajia kuajiri walimu wengi na wanalenga kupata walimu wa sayansi na hisabati.

"Pale kwenye mahitaji makubwa, kama shule ambayo haina mwalimu wa Hesabu, Fizikia na Kemia tutazingatia maeneo yenye uhitaji mkubwa wa walimu hawa," alisema.

Alibainisha kuwa serikali imepanga kupeleka walimu wa shule za msingi kwenye maeneo yenye uhitaji mkubwa.

"Tukipata kibali mwezi wa tano au wa sita, tutazingatia pia, ni kweli kuna upungufu mkubwa," Waitara alisema.

Katika swali la msingi, Bura alihoji ni lini serikali itapeleka walimu wa kutosha wa sayansi mkoani Dodoma kutokana na kuwa na upungufu wa walimu 527.

Katika majibu yake, Waitara alisema jiji hilo jipya lina shule 221 za sekondari zikiwa na wanafunzi 72,254 na mahitaji ya walimu wa sayansi na hisabati ni 1,641.

Alibainisha kuwa waliopo ni 916, hivyo upungufu ni walimu 527 sawa na asilimia 32 ya mahitaji halisi.

"Mpango wa serikali ni kuendelea kuajiri walimu wa masomo hayo kwa awamu na kwa sasa, kibali cha kuajiri walimu 4,549 kimetolewa ambapo kati ya hao, walimu 1,374 ni wa masomo ya sayansi na hisabati," alisema.

Aliongeza kuwa taratibu za kuajiri walimu hao zinakamilishwa ili kuwapanga walimu hao katika halmashauri zenye upungufu mkubwa zikiwamo Halmashauri za Mkoa wa Dodoma.

# 'Asiyejulikana' utekaji anaswa




Habari zote na Augusta Njoji, DODOMA

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imesema hadi sasa mtuhumiwa mmoja amekamatwa kwa makosa ya utekaji nyara.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Hamad Yusuf Masauni, alitoa kauli hiyo jana bungeni jijini Dodoma alipojibu swali la Mbunge wa Wingwi, Juma Kombo Hamadi (CUF).

Mbunge huyo alisema vitendo vya utekaji wa watu wasio na hatia na kuwatesa, kuwahujumu hata kuwaua, vinaendelea kukithiri nchini.

"Je, serikali ina mkakati gani wa kuzuia, kulinda na kuhakikisha inakomesha vitendo hivyo haraka sana? Je, hadi sasa ni watu wangapi ambao wamekamatwa na kuchukuliwa hatua kutokana na uhalifu huo?" mbunge huyo alihoji.

Katika majibu yake, Masauni alisema serikali kwa kutumia taarifa za kiintelijensia, imekuwa ikiweka mikakati mbalimbali kwa lengo la kuzuia na kukomesha vitendo vya aina hiyo na hadi sasa, mtuhumiwa mmoja amekamatwa kwa makosa ya utekaji nyara.

Alisema jukumu la msingi la serikali ni kuhakikisha raia wake wanakuwa salama wakati wote na wanaendelea na shughuli za uzalishaji mali na shughuli zingine za kijamii kwa amani na utulivu pasipo kuwa na hofu.

"Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali pale taarifa za utekaji, utesaji na mauaji zinapotolewa, lengo likiwa ni kuwabaini na kuwachukulia hatua za kisheria watu wanaojihusisha na vitendo hivyo," alisema.

Pamoja na majibu hayo ya Masauni, mbunge huyo aliuliza swali la nyongeza akihoji hatua zilizochukuliwa dhidi ya watekaji wa mfanyabiashara maarufu Mohamed Dewji 'Mo' na kupigwa risasi kwa Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu (Chadema).

"Je, pamoja na matukio haya ndo mtu mmoja tu amekamatwa na kuchukuliwa hatua? Na je, serikali ipo tayari kuunda tume ya kuchunguza matukio haya na wahusika wachukuliwe hatua," mbunge huyo alihoji.

Katika majibu yake, Masauni alisema matukio hayo kila moja Jeshi la Polisi limechukulia kwa uzito unaostahili.

"Matukio haya yapo kwenye hatua mbalimbali za upelelezi, yapo ambayo upelelezi wake umekamilika na yamewasilishwa kwa DPP," alisema.

Alisema suala la upelelezi ni mchakato na anaamini matukio hayo yatafikia hatua nzuri na haki itatendeka.





Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Irkujit, Kata ya Edonyongijape, wilayani Simanjiro, baada ya kufanya harambee ya kuchangia ujenzi wa Zahanati kijijini hapo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Askari Zimamoto kortini kwa tuhuma za rushwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ASKARI wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mbeya, Joseph Challe (39), amefikishwa mahakamani na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) wilayani Chunya kwa tuhuma za kupokea rushwa ya Sh. milioni 1.7 kutoka kwa mchimbaji mdogo wa madini, Suzan Kalani.

Mshitakiwa huyo alifikishwa mahakamani na kusomewa mashitaka ya kupokea rushwa ya Sh. milioni 1.7 kutoka kwa Suzan Kalani ambaye alidai kuendesha shughuli za uchimbaji madini bila ukaguzi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Emmanuel Lazaro, mbele ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Chunya, Alice Mkasela, alidai Challe anakabiliwa na makosa mawili ya kujipatia fedha kutoka kwa mchimbaji mdogo wa madini wilayani Chunya kinyume cha sheria.

Hata hivyo, Challe alikana kutenda makosa yote mawili na Lazaro alidai dhamana ipo wazi kwa wadhamini wawili ambao walitakiwa kuweka bondi ya Sh.milioni mbili kila mmoja na mali zisizohamishika. Mwendesha Mashtaka huyo wa Takukuru alidai mahakamani kuwa katika kesi hiyo ya jinai namba 96/2019, Challe pia alipokea Sh. milioni moja kinyume cha sheria kutoka kwa Hamad Juma, lakini mshitakiwa huyo alikana mashitaka hayo.

Lazaro alidai upelelezi haujakamilika na Hakimu Mkasela aliahirisha kesi hadi Mei 8, mwaka huu itakapotajwa tena.

Licha ya dhamana kuwa wazi, mshtakiwa alishindwa kukidhi masharti ya dhamana, hivyo kupelekwa mahabusu.

# Wachimbaji waomba msaada kwa serikali

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WACHIMBAJI wadogo wa madini katika Mji wa Mkwajuni wilayani Songwe wameiomba serikali kusaidia upatikanaji wa vifaa kinga ambavyo vitawasaidia kujikinga dhidi ya athari mbalimbali zinazotokea kwenye shughuli za uchimbaji madini.

Walitoa ombi hilo jana wakati wa mafunzo ya afya na usalama kwenye maeneo ya migodi yaliyoandaliwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (Osha).

Walisema wamekuwa wakifanya kazi kwenye mazingira magumu na hatari kwa afya yao kwa sababu vifaa vya uchimbaji wanavyovitumia ni hatari.

Mwenyekiti wa Wachimbaji Wadogo wa Madini Mkoa wa Songwe, Emmanuel Kamaka, alisema matumizi ya Zebaki katika shughuli za uchimbaji madini wameelezwa kuwa zina hatari, hivyo uwapo wa vifaa kinga utasaidia kupunguza madhara yanayopatikana kutokana na matumizi ya kemikali hiyo.

"Tunaomba serikali itusaidie vifaa kinga katika shughuli zetu za uchimbaji, kama itashindwa kutununulia basi watusaidie kutafuta wakala ambaye atakuja hapa Mkwajuni kutuuzia tupo tayari," Kamaka alisema.

Kamaka pia alieleza kufurahishwa na mafunzo hayo kwenye maeneo yao ya migodi kwa kuwa wachimbaji wamefundishwa masuala mbalimbali ya kujilinda na kukabiliana na athari zinazotokea wakati wa uchimbaji madini.

Alisema wachimbaji hao hawajawahi kupata mafunzo yoyote ya usalama na afya katika migodi yao, hivyo akaipongeza Osha kwa kuandaa utaratibu huo na kuwaomba kuwatembelea mara kwa mara kutoa elimu hiyo ambayo ina manufaa kwao.

"Tulikuwa tukiowaona Osha kama maadui kwa sababu kila mara wanapokuja wao ni kutupiga faini au kudai hela, sasa safari hii wamekuja kutoa elimu, hakika tumefurahi tunawashukuru na kuanzia sasa watakuwa marafiki," Kamaka alisifu.

Meneja Afya wa Osha, Jerome Materu, alisema katika mafunzo hayo wametoa tahadhari kwa wachimbaji kuachana na matumizi ya Zebaki kwa kuwa hatari kwa afya zao.

"Matumizi ya Zebaki ni hatari kwa afya, hivyo nawasihi wachimbaji muachane na vitu hivyo, tafuteni teknolojia nyingine ya kupata madini hata kama ni bei ghali, lakini bora kununua ili kuokoa maisha yako na kizazi chako," alisema Materu.

Alisema Osha iliamua kutoa elimu katika mikoa ya Mbeya na Songwe kwa sababu wachimbaji wadogo wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika shughuli zao ikiwa ni pamoja na uelewa mdogo wa namna ya kukabiliana na majanga migodini na vifaa vinavyotumika kwenye uchimbaji.

# Jela miaka mitano kwa wizi wa mtoto

**Na Mwandishi Wetu,** CHUNYA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya imemhukumu kifungo cha miaka mitano jela, Jordan Mgena (27), baada ya kupatikana na hatia ya wizi wa mtoto mwenye umri wa miaka miwili.

Mgena, Mkazi wa Kahama mkoani Shinyanga, alikuwa anakabiliwa na mashtaka ya kuiba mtoto mwenye jinsi ya kiume katika Kijiji cha Chalangwa wilayani Chunya.

Mwendesha Mashitaka Fredrick Ndosi alidai mahakamani mbele ya Hakimu Mfawidhi Wilaya ya Chunya, Osmund Ngatunga kuwa mshtakiwa alimwiba mtoto nyumbani kwa wazazi wake Novemba 8, mwaka jana.

Ndosi alidai Mgena baada ya kufika nyumbani, alijifanya ni mmoja wa wanafamilia hiyo akitokea Kahama na alikuwa anamtafuta baba yake mzazi baada ya kuambiwa na mama yake kuwa yuko mkoani Mbeya.

Alidai mshitakiwa alifanya kosa hilo kinyume cha sheria na alikamatwa eneo la Kambikatoto mwaka jana akiwa kwenye basi la Singida Line akirejea kwao Shinyanga.

Mmoja wa mashahidi katika kesi hiyo ambaye ni Mkuu wa Kituo cha Polisi Chunya na Mratibu Msaidizi wa Polisi, Janeth Mwakabungu, alidai alipata taarifa za kuibwa kwa mtoto na Jeshi la Polisi lilisambaza picha ya mtoto kwa njia ya simu na kuweka vizuizi vyote katika barabara zinazoingia na kutoka katika Wilaya ya Chunya.

Alidai Jeshi la Polisi lilifanikiwa kumkamata akiwa na mtoto kwenye Kituo cha Rungwa Kambikatoto kwenye basi la Singida Line akielekea kwao Shinyanga.

"Awali mshtakiwa alifika hapo nyumbani Chalangwa kwa wazazi wa mtoto akitokea Isanga jijini Mbeya ambako aliambiwa kuwa familia yake ipo Chalangwa ndipo alipokwenda hapo na kujitambulisha kuwa ni mwanafamilia na kwamba amekuja kumtafuta baba yake mzazi," alidai.

"Mheshimiwa Hakimu, mshtakiwa ni mzoefu kutokana na namna alivyotengeneza mazingira ya kuaminiwa katika familia hatimaye kufanikiwa kumwiba mtoto na kukamatwa katika basi akiwa anakwenda Mkoa wa Shinyanga."

Hata hivyo Mgena alikana kutenda kosa hilo, akidai kuwa siku ya tukio la kukamatwa, mtoto huyo alikuwa na shangazi yake aitwaye Helena Kahawa, hivyo hahusiki na wizi wa mtoto.

Baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili, Hakimu Ngatunga alisema mahakama imemtia hatiani na kabla ya kutoa hukumu alimpa nafasi ya kujitetea.

Katika utetezi wake, Mgena alidai hilo ni kosa la kwanza, mke wake ana mtoto mdogo na mama yake ni mgonjwa, hivyo akaomba apunguziwe adhabu kwa kuwa wanamtegemea.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Ngatunga alisema mahakama inamhukumu kifungo cha miaka mitano jela ili iwe fundisho kwa watu wenye tabia kama hiyo na rufaa ipo wazi kwa upande usioridhishwa na uamuzi huo.





# Washauriwa kutumia rasilimali kuibua miradi

**Na Paul William,** MOSHI

WAJASIRIAMALI wadogo mkoani Kilimanjaro, wametakiwa kutumia rasilimali zilizopo na fursa zinazojitokeza kuibua miradi ya biashara na kuendesha biashara zao kitaalamu kwa lengo la kujikwamua na umaskini.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi wa Taasisi ya Tanzania Youth Enquipping Organization (TAYEO), Joseph Ngomite, wakati akizungumzia uzinduzi wa tamasha la kampeni yenye kauli mbiu ya "Badilika na Tanzania Inayobadilika".

Ngomite alisema katika tamasha hilo, ambalo litazinduliwa kesho na Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, zaidi ya vijana 100 wanatarajiwa kuhudhuria mafunzo hayo ya Mtazamo, Fursa na Uweshaji kwa Vijana vyuoni na mitaani.

Alisema: "Vijana katika taifa letu ndio nguvu kazi kubwa ya taifa, kwa takwimu zilizotolewa hivi punde Bara la Afrika linaonekana litakuwa na vijana wengi sana, ukuaji wa vijana utakuwa mkubwa, ukilinganisha na mabara mengine," alisema Ngomite.

Alisema TAYEO, inayojishughulisha na makundi ya vijana, imeangalia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, ambayo sio mbali ni miaka sita tu ijayo.

"Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, nchi yetu inaelekea kwenye uchumi wa kati, hivyo tumeona kama serikali tutaiachia peke yake kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango, haziwezi kufanya kazi pasipo sisi vijana kuingia na kufanya kazi hizo," alisema.

Alisema malengo ya kampeni hiyo ni kutambua na kuitengeneza nguvukazi kubwa ya taifa ambayo ni vijana wawe na mtazamo chanya, waweze kutumia fursa na uwezeshaji na kuwa sehemu muhimu kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

Alisema serikali ya awamu ya Rais John Magufuli imefungua milango ya kuwasaidia wajasiriamali wadogo kwa kutumia fursa zilizopo, hivyo aliwataka vijana kuibua miradi ya biashara na kuwa na utayari wa kukabiliana na changamoto zilizopo katika biashara.

Alisema malengo ya tamasha hilo ni kutambua na kuitengeneza nguvukazi kubwa ya taifa ambayo ni vijana wawe na mtazamo chanya, waweze kutumia fursa na uwezeshaji na kuwa sehemu muhimu kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.



Meneja wa Bandari ya Tanga, Percival Salama (kushoto), akifafanua jambo kwa waandishi wa habari wa mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, waliofanya ziara ya kuona shughuli zinazofanywa katika bandari hiyo, jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Viongozi dini waonyeshwa fursa za uchumi

**Na Paul William,** MOSHI.

WITO umetolewa kwa viongozi wa dini ya Kiislamu katika mkoa wa Kilimanjaro, kubuni na kuanzisha miradi ya kiuchumi, ikiwamo ya kilimo na ufugaji ili kuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato.

Hayo yalibainishwa na mshauri wa mambo ya uchumi wa Baraza la Waislamu Tanzania mkoa wa Kilimanjaro (BAKWATA), Ibrahim Shayo, alipokutana na kuzungumza na uongozi wa misikiti kutoka wilaya za Siha, Moshi na Hai.

Shayo aliwashauri kuanzisha miradi maarifa ya kuanzisha biashara itakayowawezesha kupunguza utegemezi wa wafadhili kutoka nje badala yake wabadili fikra na kuanzisha miradi katika misikiti yao ikiwamo ile ya ufugaji wa samaki, ufugaji wa nyuki na mengineyo.

"Nawaombeni Maimamu walioko kwenye misikiti, anzeni kubadili fikra zenu kwa kuanzisha miradi ya kilimo na ufugaji, naamini kwa kufanya hivyo mtakuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato, itakayowezesha katika kusukuma mbele maendeleo ya Waislamu," alisema Shayo.

Shayo ambaye pia ni Mkurugenzi wa mabasi ya IBRA LINE, aliwataka Maimamu wa kila msikiti kuchangamkia fursa zilizopo kwenye maeneo yao kwa kuanzisha miradi ya kiuchumi, itakayowasaidia kuleta mapato ya uhakika na kuondokana na hali ya kuwa ombaomba.

Aliwaasa viongozi wa Kiislamu kuachana na migogoro ya mara kwa mara kwenye misikiti badala yake waanzishe miradi ambayo itaweza kuwakwamua kiuchumi.

Akizungumza kwenye kikao cha viongozi hao wa dini, kilichowakutanisha Maimamu wa misikiti pamoja na Masheikhe wa wilaya za Moshi na Siha, Katibu wa BAKWATA wilaya ya Moshi, Sheikh Nuhu Mnango, amewataka Maimamu pamoja na walimu wa Madrasa kujenga upendo ili kuondoa migogoro miongoni mwao.

Mjumbe wa Baraza la Ulamaa Taifa, Sheikh Shaaban Rashidi, amewataka Waislamu kujitoa kwa ajili ya maendeleo ya waislamu na Uislamu nchini.

## Halmashauri zabebeshwa zigo la migogoro ya ardhi

**Na Mary Mosha,** SAME

SERIKALI mkoa wa Kilimanjaro imesema migogoro kati ya wakulima na wafugaji imekuwa ikichangiwa na baadhi ya wataalamu wa ardhi katika halmashauri.

Sababu zilizotajwa ni kushindwa kuelimisha jamii, kutenda haki pamoja na kuweka matumizi bora ya ardhi. Akizungumza na wananchi wa kijiji cha Marwa Wilaya ya Same, Mkuu wa Mkoa huo, Amma Mghwira , alisema serikali haitasita kuwachukulia hatua wataalamu katika idara mbali mbali ikiwamo ya ardhi ikiwa watashinwa kuwa chachu ya kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji.

Alisema katika halmashauri baadhi ya wataalamu ambao sio waaminifu wamekuwa chanzo cha migogoro kutokana na kushindwa kuweka matumizi bora ya ardhi pamoja na kutoa elimu kwa wakulima juu ya madhara hayo ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima. "Baada ya kuongea na kuwasikiliza wakulima na wafugaji tumebaini kuwa wapo baadhi ya wataalamu wetu ambao wamekuwa chanzo cha migogoro kutokana na kushindwa kusimamia sheria na taratibu zilizowekwa pamoja na kupokea rushwa ili kupindisha ukweli hasa wanapofika vijijini," alisema na kuongeza:

"Nawaagiza watendaji wote katika halmashauri zote mkoa kuhakikisha wanalitazama suala la wakulima na wafugaji katika kuweka sawa matumizi bora ya ardhi wakionyesha eneo la malisho na la wakulima ili kupunguza migogoro.: Katika hatua nyingine, Mghwira aliwataka viongozi wa vitongoji na vijiji kuainisha njia kwa ajili ya mifugo pamoja na kuchimba mabwawa ambayo yatatumika kwa ajili ya majosho ya mifugo.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Majid Kabyemela, ambaye ni Ofisa Kilimo na Mifugo wilayani humo, alisema halmashauri hiyo imetenga kiasi cha Sh. milioni 25 kwa ajili ya kufanya mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vinne vya Kata ya Ruvu.

Alisema migogoro kati ya wakulima na wafugaji inachangiwa kwa kiasi kikubwa na uwapo wa mifugo mingi katika eneo hilo, na kwamba Kata ya Ruvu pekee inaongoza kwa kuwa na mifugo mingi katika Wilaya ya Same.

Katibu wa baraza la usuluhishi migogoro ya ardhi Kata ya Ruvu, Nangala Koole Mollel, alisema kutokuwapo kwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji kunasababisha migogoro hiyo.



Ukurasa 18

Madereva wasafirishaji mafuta nje walia kusingiziwa dhuluma



Ukurasa 19

Mtihani wa kinamama kufikia '50 kwa 50' katika ujasiriamali



Ukurasa 14

## TBS ilipotua ghafla Mbeya ikaibua 'madudu' viwandani, sokoni, madukani


# BUFE

Ijumaa Aprili 26, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 16

## Muungano unavyowashia uchumi wa Watanzania 'taa ya kijani'


KIBIASHARA ZAIDI Ukurasa 19

Madereva walia kusingiziwa dhuluma Ukurasa 18

**Muhtasari wa Soko**

**Kielezo**

| | |
|---|---|
| TSI | 3,482.82-0.18 |
| DSEI | 2,020.08-12.15 |

## Biashara

Jumla ya Mauzo (bln) 20,191.48

| | |
|---|---|
| Mauzo | 16,751,775.00 |
| Hisa | 19,471.20 |

**ZILIZOPANDA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| KCB | 900 | +1.12% |
| NMG | 1,540 | +1.32% |
| ACA | 4,640 | +-6.26% |
| EABL | 4,380 | ++0.83% |
| JHL | 9,250 | - +1.09% |

**ZILIZOSHUKA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| ACA | 5,290 | 0.38% |
| KA | 110 | -4.35% |
| NMG | 1,530 | -0.65% |
| KCB | 870 | -1.14% |

BIASHARA

# TBS ilipotua ghafla Mbeya ikaibua 'madudu' vi

- Mkoa wajengwa kutumia mabati feki
- Wagundua viwanda vinavyowakaidi
- Mitumba, vifaa magari

**Nebart Msokwa**, MBEYA

MWEZI uliopita, Shirika la Viwango Tanzania (TBS), liliendesha operesheni maalumu kukagua maduka yanayouza bidhaa mbalimbali, maghala ya kuhifadhi na viwanda vinavyozalisha jijini hapa.

Lengo lilikuwa kuondoa bidhaa zisizokidhi viwango, pia kutumia sheria kuwachukulia hatua wauzaji na wazalishaji, lengi ni kukomesha biashara hiyo na kuwaondolea wananchi hatari ya madhara.

Ni operesheni iliyoendeshwa na maofisa wa TBS makao makuu, Dar es salaam walioshirikiana na watokao Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, pia Jeshi la Polisi. Ni ukaguzi wa kushitukiza kwenye masoko na viwanda vya Mbeya.

**Viwandani**

Walianzia viwanda vitatu vya kutengeneza mabati na ghala la kampuni, pia baadhi ya maduka ya vifaa hivyo, yaliyopo maeneo ya Ottu na Sido, walikonasa mabati feki 2004 yenye migongo mipana.

Ni mabati yaliyozalishwa viwandani, yakigundulika kuwa na viwango vya chini, Waliwaagiza wamiliki wa viwanda hivyo ama wasiyauze au kuendelea kuzalisha, kama mikataba yao inavyowataka.

Ofisa Uhusiano wa TBS Makao Makuu, Roida Andusamile, anasema Sheria za Viwango Tanzania, inataka bati zote za migongo mipana zitengenezwe kuanzia geji 28 au chini ya hapo, lakini zilizokamatwa zilikuwa na geji 30.

"Wamezalisha na ndio maana tumeyazuia na tutawachukulia hatua zingine za kisheria, ili kukomesha biashara hizi," anasema Roida

Mkaguzi Ubora wa TBS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Yekonia Sanga, anasema wazalishaji hao wamekiuka kiwango anachokitaja; Namba TZS 1476 cha Mwaka 2012, kinachowazuia kuzalisha bati kiwango hicho.

Anasema, mabati hayo kwa jumla yana thamani ya Sh. milioni 60 na anawatahadharisha wazalishaji kuacha kuchezea sheria za nchi.

Mhandisi Sanga anafafanua, katika ghala la kampuni moja TBS imekamata mabati 800; kiwanda kingine mabati 500; na kuna kiwanda yamekutwa mabati 704, anazoahidi zote zitateketezwa baada ya taratibu kukamilika.



Maofisa wa TBS, wakikagua mabati jijini Mbeya, ambako walikamata bati 500 za migongo mipana, zisizokidhi viwango na kuzichukua.

> **"Hatua ya kwanza tumezuia bati hizi na tumewasainisha zuio la kutoziuza tena. Wana siku 14 za kuwasilisha utetezi wao kwa Mkurugenzi Mtendaji wa TBS. Baada ya hapo itafahamika kama wanalipa faini au wanapelekwa mahakamani**

Mhandisi Sanga anaeleza, baada ya operesheni ya Mbeya, walielekea mkoani Rukwa na wakiwa njiani, wakipata taarifa za siri kuwapo baadhi ya viwanda vilivyoendelea kuzalisha na kuuza mabati yasiyokidhi viwango.

Anasema, kutokana na taarifa hizo walirudi jijini Mbeya walikokuta zaidi ya bati 1000 mpya zikiendelea kuuzwa, ambazo zilibebwa zote kuhifadhiwa katika ghala la TBS kusubiri taratibu za uteketezaji.

Mkaguzi ubora kutoka TBS makao makuu, Baraka Mbajije, anaahidi kuchukuliwa hatua za kisheria, huku akilalamika kuwapo matumizi mabaya ya nembo yao ya ubora.

Ananukuu vifungu vya kisheria, akieleza adhabu zinazoelekeza wazalishaji kutozwa faini mbalimbali, ikiwamo isiyopungua Sh. milioni 20, kwa anayepatikana na kosa la matumizi mabaya ya nembo ya ubora na akakiri kosa papo kwa hapo.

Mbajije anaongeza, dai la kosa hilo linapofika mahakamani, adhabu inaongezeka kufika kati ya Sh. milioni 50 na 100.

"Hatua ya kwanza tumezuia bati hizi na tumewasainisha zuio la kutoziuza tena. Wana siku 14 za kuwasilisha utetezi wao kwa Mkurugenzi Mtendaji wa TBS. Baada ya hapo itafahamika kama wanalipa faini au wanapelekwa mahakamani," anasema Mbajije.

Baadhi ya wafanyabiashara wanalalamika uuzaji mabati feki umechangia biashara kuwa ngumu kwa wauzao mabati yenye viwango, kwani wauzaji feki bei zao ni ndogo.

Mwakilishi wa kampuni ya GS Group, Seif Abdi anakiri, viwanda vinavyozalisha bati feki zimechangia wateja kupungua kwenye maduka ya yenye bidhaa halali.

"Wenzetu wanaozalisha mabati feki na kuuza kwa bei ya chini, wametupotezea wateja wetu. Hivyo, tunawashukuru TBS kuendesha ukaguzi huu," anasema Abdi.

**Nguo za ndani**

Baada ya ukaguzi wa vifaa vya ujenzi, maofisa hao wa TBS walivamia soko la Sido jijini Mbeya, ambako ni maarufu kwa uuzaji nguo za mitumba, Pia, walikowakuta wafanyabiashara wakiukaji sheria.

Ni ukaguzi wa madukani ul-



Mkaguzi Ubora wa
Sido, jijini Mbeya.

ioangu
ndani
zilizoe
ozikus
wa po
20 ya 
ghalan
ri tarat
Ni m
wafany
maduk
Mka
makao
ma k
wanao
pigwa
panya,
moto z
Mba
TBS i
ya ku
kwend
vuruga
mwish
hurika
"Tu
na kw
sababu
nazo
Tunap
likozic

BIASHARA

**Muungano unavyowashia uchumi wa Watanzania 'taa ya kijani'**

Ukurasa 16

BIASHARA

**Mtihani wa kinamama kufikia '50 kwa 50' katika ujasiriamali**

Ukurasa 19

BIASHARA

**Madereva wasafirishaji mafuta nje walia kusingiziwa dhuluma**

Ukurasa 18


# iwandani, sokoni, madukani



TBS, Baraka Mbajije, akikusanya baadhi ya nguo za ndani za mitumba walizokuta zinauzwa katika soko la **PICHA ZOTE: NEBART MSOKWA.**

ukia nguo za mitumba za zilizopigwa marufuku, ndelea kuuzwa. Wali-anya chini ya usimamizi lisi, zaidi ya marobota nguo hizo, zilizopelekwa ni anakosema zinausubi-tibu za uteketezaji.

nkasa ambao, baadhi ya yabiashara walifunga ka yao na kutimua mbio. guzi Ubora wa TBS makuu, Mbajije, anase-kuna wafanyabiashara ingiza nguo hizo zilizo-marufuku kupitia nja za , hali inayowapa changa-za udhibiti.

jije anasema, hivi sasa meanzisha operesheni zikamata nguo sokoni, la kuziteketeza, ili ku-a soko la watumiaji wa o, ambao ndio wanaod-zaidi.

naamua kuzichukua enda kuziteketeza kwa u hawa tunaowakamata hawatupi ushirikiano. owataka waeleze wa-hukua, sasa wakiingia hasara hivi ndio wataanza kuogopa kuziuza," anaeleza Bajije.

Anasema, kwa sasa wanasubiri taratibu ziwekwe vizuri, wakimkuta anauyeuza nguo hizo, anakamatwa na kupelekwa mahakamani, badala ya kuishia kuteketeza nguo hizo.

Ofisa Uhusiano, Roida, anataja madhara ya nguo hizo kwa wanunuzi wanaotumia ni magonjwa ya ngozi, akisema ndio sababu serikali imepiga marufuku uingizaji wa nguo hizo na kutunga sheria za kusimamia jambo hilo.

Roida anasema, TBS itaendelea na ukaguzi wa kushitukiza wa maeneo mbalimbali nchini, ili kuzikamata na kuziteketeza nguo hizo, pia kuwachukulia hatua wahusika, ili biashara hiyo ikomeshwe.

"Hizi nguo zina madhara, lakini baadhi ya Watanzania wenzetu wanazikimbilia. Tujiulize, kwanini hata wewe ukivaa nguo hizi za ndani ukaichoka unaitupa, badala ya kumpa mdogo wako aendelee kuivaa? anahoji Roida.

Anawataka wananchi kutoa taarifa kwenye mamlaka za serikali, ikiwamo TBS na Polisi, pindi wanapoona uingizaji kabla hazijafika sokoni.

Vilainishi feki.

Pia, ukaguzi wa kushitukiza ulitua kwenye maduka ya vilainishi vya magari visivyokidhi viwango bora. Katika maeneo ya Soweto, Kabwe na Mwanjelwa na maghala ya kuhifadhi vilainishi, yaliyopo katika majengo ya Ottu.

Huko nako, TBS ilikamata bidhaa feki, zikiwemo shehena za vilainishi vya mifumo mbalimbali ya magari na zilichukuliwa kwa ajili ya uteketezaji. Baadhi zilikutwa zimefichwa kwa ajili ya mauzo ya siri.

Mkaguzi Ubora wa TBS, Mhandisi Sanga, anafafanua kuwa ni vilainishi vilivyopigwa marufuku nchini, kwa sababu ya kukosa uwezo wa kufanya kazi inayokusudiwa kwenye vyombo vya moto.

Anavitaja vilivyokamatwa kwa viwango anavyotaja 'DOT 3' vilivyotumikwa kwenye magari na kusababisha ajali, kutokana na mifumo ya breki kushindwa kufanya kazi yake.

"Vilainishi vya aina hii nguvu yake ni ndogo kwa sababu vinapata moto haraka. Vikishachemka, vinaaza kutoa mvuke ambao unabadilika na kuwa maji, ambayo yanarudi tena na kuchanganyika na mafuta. Hapo ndio mafuta hayafanyi kazi tena," anaeleza Mhandisi Sanga.

Anaeleaza, baadhi ya ajali zinatokea kutokana na matumizi ya vilainishi hivyo, lakini wanaohukumiwa ni wengine, wakiwamo madereva na maofisa wa Polisi.

Roida anaahidi, wataendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara na watumiaji vilainishi, kuhakikisha biashara hiyo haramu inakomeshwa nchini na kubaki historia.

Baadhi ya wafanyabiashara wanaouza vilainishi aina hiyo, wanadai kuwa uwepo wa vilainishi feki unasababishwa na bidhaa zao kukosa soko.

# Bosi Nissan kikaangoni kwa dai la ufisadi

**Tokyo, Japan**

NI mtihani kwa mabosi wa kampuni kubwa za magari duniani, kuangukia mkono wa sheria.

Wakati Ijumaa iyopita jarida na safu hii ilikuwa na simulizi ya aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya magari ya Volkswagen huko Ujerumani akitua mahakamani, akishitakiwa magari yake kuchafua hali ya hewa, huko Japan nako kuna mambo.

Mahakama ya jijini Tokyo, jana ilitoa dhamana kwa aliyekuwa bosi wa kampuni ya magari ya Nissan, aliyekuwa ndani akidaiwa kutumia vibaya fedha za ofisi.

Carlos Ghosn, alipewa dhamana ya Yen miloni 500 au sawa na zaidi ya Sh. Bilioni moja, akikabiliwa na mashitaka manne yanayoangukia katika ulaji pesa.

Ghosn, mwenye umri wa miaka 65, mwanzo alitiwa mbaroni na kisha akaachiwa, kabla ya kukamatwa tena na kupadishwa kizimbani tarehe 4 mwezi huu.

Inadaiwa alikula njama za ulaji pesa, kwa kulipa mamilioni ya dola huko kwa wakala nchini Oman, lakini ikagundulika Dola za Marekani milioni tano sawa na Sh. bilioni 11.15 ziliingizwa tena katika akaunti yake binafsi.

Ghosn alitiwa mbaroni kwa mara ya kwanza Novemba mwaka jana na alikuwa rumande kwa siku 108 (miezi mitatu na nusu), kisha akatoka kwa dhamana ya Dola za Marekani milioni tisa (Sh. bilioni 20.07).

Ghosn anafahamika kuwa mahiri katika kupaisha uzalishaji magari. Pia, katika vita vya masoko ya magari iliyohusika magari ya Nissan anayozalisha, Renault ya Ufaransa na Mitsubishi ya Japan mwaka 2016, ujuzi wake ulitumika sana.

Katika utetezi wake mhakamani, Ghosn anasema zote ni njama chafu dhidi yake. a kimaadili kwa watoto kuamini katika hekaya hizo na kisha akapiga picha na Father Christmas na kuirusha kwenye mtandao wake wa Twitter na kuandika kuwa anaamini (kuwa yupo).



Carlos Ghosn; bosi wa zamani wa Nissan.

**BEI YA MAZAO >>** MCHELE 184375 | ULEZI 142642.9

**FEDHA >>** RAND 159.8062| KSH 22.6251|USH0.6152

UCHUMI

# Muungano unavyowashia uchumi wa Watanzania 'taa ya kijani'

**Na Peter Orwa**

LEO kunaadhimishwa miaka 55 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, iliyozaa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, waasisi wakiwa Mwalimu Julius Nyerere wa chama cha TANU na Sheikh Abeid Amaan Karume kutoka Afro Shirazi Party (ASP).

Pande zote mbili za muungano, ziko katika sura ya bashasha katika hilo, isipokuwa kwa machache yaitwayo 'Kero za Muungano' ambazo zinafanyiwa kazi katika sura ya pande mbili.Vipo vyombo maalum katika hilo.

Historia ya Muungano ni kubwa na kuna mengi mazuri yanayoelezeka kutoka kwa waasisi ambao wengi wamekwishatangulia mbele ya haki.

Katika kutathmini sura ya mafanikio kuna yaliyorasmi na katika maandishi na yasiyo rasmi. Lakini katika jibu la majumuisho yanaagukia katika 'mazuri' kupitia nyanja nyingi za sekta na mifumo ya maisha ya kawaida.



Ujenzi wa barabara mpya ya lami kisiwani Pemba, makutano ya Mabao kuelekea Kengeja na Uwanja wa Ndege wa Karume, Chakechake. **PICHA: MTANDAO.**

**MIRADI YA MAENDELEO**

Inapoangaliwa kiuchumi kuna mengi yasiyohesabika, hasa katika sura ya kuandaa maendeleo ya nchi, mbali na historia ya kuwapo miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa makazi, maghorofa eneo la Michenzani na Pemba katika zama za uongozi marehemu Sheikh Abeid Amaan Karume.

Vivyo hivyo, kuna mifano ya kazi za namna hiyo, ambazo zimefanywa katika zama za karibuni katika uongozi wa Rais Amaan Karume na baadaye, Dk. Ali Mohmmed Shein.

Sura pana inachukua nafasi katika suala la raia wa pande mbili kuhijhusisha katika majukumu mbalimbali ya kiuchumi, ikiwamo Wazanzibari mbalimbali akiwa wakazi wa Tanzania Bara, baadhi wamejikita katika kilimo, mfano hai walimaji na wafanyabiashara wa mpunga walioko wilayani Kyela, mkoani Mbeya.

Zanzibar kumepiga hatua katika miradi ambako sasa ni kitovu kikubwa cha utalii wa kihistoria, hoteli nyingi zimejengwa zikisheheni wahudumu kutoka Tanzania Bara.

Pia, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Abeid Amaan Karume, imekuwa kitovu kiunganishi cha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam, kutokana na kuwepo uhusiano mkubwa wa kibiashara.

> **"Zanzibar kumepiga hatua katika miradi ambako sasa ni kitovu kikubwa cha utalii wa kihistoria, hoteli nyingi zimejengwa zikisheheni wahudumu kutoka Tanzania Bara.**



Wanafunzi katika Chuo cha Ualimu Benjamin William Mkapa na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mchanga Mdogo, wakimsikiliza Rais wa Zanzibar, Dk.Ali Mohamed Shein (hayupo pichani), alipozindua tawi la Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), chouni hapo. **PICHA: IKULU SMZ.**

Katika picha ya mwonekano wa kushabiliana na ujumbe wa kibiashara, wakati Uwanja wa Ndege uliopo Zanzibar upanuzi wake ulikamilika si miaka mingi iliyopita, hicho hicho ndicho kiko katika hatua ya mwisho kwa uwanja wa Dar es Slaaam.

Hivi sasa sehemu kubwa za ndege za kimataifa, zinasafiri kati ya viwanja vya ndege vya Dar es Salaam, kukiwapo abiria wengi kati ya vituo hivyo viwili.

Mtazamo huo ndio umeteka sana sekta ya usafiri majini, kukishuhudiwa upanuzi wa bandari za pande zote mbili za Muungano na kuongezeka kwa shughuli za umma.

Sehemu kubwa ya abiria, pia bidhaa na masoko yake ni kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, ambayo inarejesha ishara ya Muungano.

Miaka miwili kabla ya kumalizika awamu ya uongozi uliopita, Rais Dk. Shein alikaribisha wanahabari kutoka pande mbili za Muungano, kuwatangazia mafanikio ya kukamilika malengo yake binafsi na ilani ya uchaguzi aliyoingia nayo katika awamu hiyo.

Ni zama inayoshuhudiwa mageuzi makubwa, kama ya kupanuka Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) ambacho sasa kina mafunzo mengi hadi ngazi ya uzamili. Zamani, Wazanzibari walipata elimu ya juu kutoka Bara, ikiwamo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaaam.

Mradi mwingnie, anautaja Dk. Shein ni Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, kupanuka kwa kasi, ikiendana na ongezeko la madaktari, wakiwamo wanaotoka nchini Cuba.

Nipashe ni miongoni mwa mashuhuda wa shule nyingi za sekondari na chuo cha ualimu kuanzishwa Unguja, huku Pemba ambako ni kitovu cha uzalishaji karafuu, uchumi na soko lake limeboreshwa maradufu, ikiwamo kiwanda na kudhibiti bei na usafirishaji nje kinyemela .

Dk. Shein katika wasaa huo huko Pemba, alizindua mradi wa barabara mbalimbali unaofika vijijini ambako kulikuwa na hali mbaya ya usafiri wa ndani, chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

Taarifa ya kiserikali

Katika mawasilisho ya kiserikali kuhusu mafanikio ya Muungano, kulitajwa sera na sheria ya moja ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ya mwaka 1995, imekuwa kichocheo cha kukua uchumi kwa pande zote za Muungano.

Inaonyeshwa kuwa ni hali iliyowezesha kushuka mfumuko wa bei kutoka asilimia 30 katika miaka ya 1990 hadi chini ya asilimia 10.

Pia, uchumi unaelezwa kuongezeka kila mwaka, sambamba na mikopo kwa sekta binafsi, benki na taasisi mpya za fedha zimeanzishwa nchini kwa pande zote za Muungano.

Katika hilo kuna miradi mingi ambayo serikali inaitaja inashirikiana kubuni na kuibua kwa ufadhili wa kiserikali, pia kushirikiana na wahisani wa maendeleo.

Mfano mmojawapo ni Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF, ambayo inayooshewa kidole ya kuwa chachu kubwa ya maendeleo ndani ya Muungano.

Kuimarika usafiri na usafirishaji na uboreshaji miundombinu katika sekta ya usafiri, kunaelezwa kumeendelea kufanyika, hususan katika ujenzi wa barabara, miundombinu ya umeme na maji.

Hiyo inaelezwa kuwa iko sambamba na ungezeko la huduma za usafiri wa anga na majini, kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, ikiwarahisisishia wananchi usafiri.

**Umoja wa Majanga**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), zimejiwekea mfumo wa kushirikiana na mamlaka za kiraia, taasisi za Muungano na watu binafsi kukabili majanga yanayozikumba nchi, ikirejewa mfano wa mkasa kuzama meli ya MV Spice Islanders, zaidi ya miaka nane sasa katika Mkondo wa Nungwi

**Uchumi ulivyosimama**

Kwa kurejea habari iliyochapishwa na Shirika la Habari Uingereza (BBC), Mei 7 mwaka jana, inasema Tanzania imeorodheshwa kuwa miongoni mwa mataifa ambayo uchumi wake utakua kwa kasi zaidi, kufikia mwaka 2026, kwa mujibu wa Kituo cha Kimataifa cha Maendeleo cha Chuo Kikuu cha Havard, Marekani.

Tanzania itakuwa ya nne kwa uchumi wake kukua kwa kasi zaidi kufikia wakati huo, ikikadiriwa kushika nafasi ya nne. Makadirio ya ukuaji ya kituo hicho, yalifanywa kwa kutumia mchangamano wa kiuchumi.

Ripoti hiyo ya Havard ilibaini kwamba kampuni ambazo zimefanya mabadiliko chanya na kuingiza uchangamano katika sekta mbalimbali za uchumi kwa mfano India na Vietnam ndizo zitakazokua kwa kasi zaidi katika mwongo mmoja ujao.

Kwa mujibu wa ubashiri huo wa kiuchumi, takwimu za orodha ya mataifa 15 ambayo yanayokadiriwa kuongoza kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kufikia 2026:

| NA. | TAIFA | UKUAJI UCHUMI KWA % |
|---|---|---|
| 1 | INDIA | 7.89 |
| 2 | UGANDA | 7.46 |
| 3 | EGYPT | 6.63 |
| 4 | TANZANIA | 6.15 |
| 5 | INDONESIA | 6.13 |
| 6 | KYRGYZSTAN | 6.04 |
| 7 | PAKISTAN | 5.99 |
| 8 | VIETNAM | 5.89 |
| 9 | MALI | 5.89 |
| 10 | KENYA | 5.87 |
| 11 | PHILIPPINES | 5.75 |
| 12 | MADAGASCAR | 5.73 |
| 13 | SENEGAL | 5.7 |
| 14 | LIBERIA | 5.7 |
| 15 | TURKEY | 5.57 |

Katika takwimu nchi za ubashiri wa wasomi wa Chuo Kikuu cha Havard, kunashuhudiwa katika mataifa ya Afrika Mashariki, kuna wafanyakazi wanaoacha kilimo na kuingia kwenye sekta ya viwanda.

Pia, wanasema bidhaa zinazouzwa nje kutoka mataifa Afrika Mashariki inaongezeka, huku sehemu ya ukuaji unatarajiwa uchumi kuchangiwa na ongezeko la watu.

Ni kiatu cha Muungano na soksi ya amani, ndizo zinaoiweka taifa la Tanzania na wananchi wake katika mtazamo huo.

# Biashara katika picha



Ofisa Madini mkazi wa Mkoa wa Kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima (kulia), akimuonyesha Waziri wa Madini, Dotto Biteko (wa tatu kushoto), eneo la machimbo ya madini ya Tanzanite Mji mdogo wa Mirerani alipotembelea jana. **PICHA: GIFT THADEY**



Mdau wa elimu na Mfanyabiashara, Erick Emmanuel (wa tano kushoto), akikabidhi mifuko 25 ya saruji kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, kwa ajili ya kusaidia kupunguza changamoto ya ukosefu wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari wilayani humo, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: SHABAN NJIA**



Muuza pipi akiwa 'ameuchapa' usingizi wakati akisubiri wateja katika eneo la ukuta wa Shule ya Msingi Daimond, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA**: **MIRAJI MSALA**

**BEI YA MAZAO >>** MAHINDI 52625-| MAHARAGE 170000.0

BIASHARA

# Madereva wanaosafirisha mafuta nje walia kusingiziwa dhuluma

- Vipimo vya 'stiki' nchini, nje mita
- Waziri Biashara aahidi kuliingilia

**Na Sabato Kasika**

MADEREVA wa malori yanayosafirisha mafuta nje ya nchi, wametoa kilio chao kwa serikali wakiomba itangaze rasmi vipimo halali vinavyotumika kupima mafuta hayo, ili kuwaondolea usumbufu wanaopata.

Hivi karibuni madereva hao zaidi ya 200 walikutana katika mkutano maalum jijini Dar es Salaam, kujadili changamoto zinazowakabili na wakakubaliana kwamba, kuanzia sasa hawataki mafuta yapimwe kwa mita.

Mkutano huo uliitishwa na Chama cha Wafanyakazi wa Malori Tanzania (Chawamata), ambayo wanachama walitoa dukuduku zao, kilio kikuu kikiwa upimaji mafuta kwa kutumia mita.

Mwenyekiti wa chama hicho, Michael Wimilie, anasema mara nyingi mita huwa zinachezewa, hivyo hawaziamini na badala yake wanataka kitumike kipimo cha 'stiki' anachoamini hakiwezi kuchakachuliwa.

Tatizo hili ni la muda mrefu na tunakumbana nalo nje ya nchi, sisi madereva wa Tanzania, lakini wenzetu wa nchi nyingine mafuta yao yanapimwa kwa 'stiki' cha ajabu sisi tunalazimishwa kutumia mita," anasema Wimile.

Anaeleza anaamini vipimo vya mita vimekuwa 'vikichezewa' ili idadi ya lita za mafuta walizobeba zionekane ndogo dhidi ya kilichoandikwa kwenye fomu, hivyo wao kuonekana wameiba mafuta, kumbe siyo sahihi.

Wimile anasema, ni hali inayowaweka katika matatizo makubwa kwa waajiri wao, kwani wamelivumilia na inawakwaza, wanalazimika kupaza sauti ya kukataa.

**KILIO CHAO**

Mwenyekiti huyo anasema, vipimo vya mita mara nyingi vinaoonyesha kuwa lita za mafuta walizobeba ni pungufu, husababisha waajiri wao wawalipishe, kuwataka posho na mishahara ili kufidia hasara.

"Hali kama hiyo imesababisha baadhi ya madereva kufungwa, kwa tuhuma za wizi wa mafuta, wengine kupata msongo wa mawazo na hata kusababisha ajali wawapo barabarani na matatizo mengine mengi," anasema.

Anafafanua woga wao kwamba changamoto hizo ambazo zinatishia maisha yao, hata kuwafanya wakutane na kuazimia kudai 'stiki' ndizo zitumike kupima mafuta.



Malori kama hili yamekuwa yakisafirisha mafuta mikoa mbalimbali na mengine yakienda nje ya nchi.
**PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

> **"Ninaamini kwa umoja huu tutapaza sauti na serikali itasikia na kutoa tamko la kutusaidia katika vita hii ambayo kwa kweli imetumiza sana**



Mwenyekiti wa Chawamata, Michael Wimile, akizungumza mkutanoni

"Tunaiomba serikali itamke wazi kuhusu utumiaji wa vipimo hivi kwani huko nje ya nchi tunanyanyaswa sana na matokeo yake tunaonekana tunaiba mafuta na kumbe vipimo vimechezewa ili kutukomoa," anasema.

Happiness Swaga, anasema wao madereva wa Tanzania wananyanyasika kwa vipimo, hivyo mara nyingi vinaonyesha wamebeba lita pungufu za mafuta, tofauti na zilizoandikwa kwenye fomu.

"Ninaamini kwa umoja huu tutapaza sauti na serikali itasikia na kutoa tamko la kutusaidia katika vita hii ambayo kwa kweli imetumiza sana. Mbona wenzetu nchi nyingine mafuta yao yanapimwa kwa 'stiki'? anahoji.

Anasema, vipimo vya mita vimesababisha msuguano kati ya madereva na waajiri wao, hasa wale wanaojikuta wana lita pungufu za mafuta, tofauti na walizobeba.

Hivyo, Swaga anamini kukataa mita hizo zinaweza kuwaeka salama.

Angetile Mwakiyasala, ni dereva anayesema kuwa baadhi ya matatizo wanayokumbana nayo yanaanzia nchini na mwisho hali inakuwa mbaya wanapofika kushusha mafuta nje ya nchi.

"Unaweza kujaziwa mafuta katika tanki la gari wiki moja kabla ya safari, halafu nyaraka zinaandaliwa siku ya kuondoka. Utaratibu huo siyo mzuri, kwa sababu matanki ya magari ni ya kusafirisha, siyo ya kutunzia mafuta," anasema Mwakisyala.

Anasema, kule wanakopeleka mafuta hayo kuna wakati hukaa zaidi ya mwezi mmoja kabla ya kumimininwa na kwamba katika mazingira hayo, kuna uhakika mkubwa wa mafuta kupungua.

"Mafuta yanapungua, kwa sababu matenki hayo haysakutengezwa maalum kwa ajili ya kuhifadhi mafuta bali kusafirishia tu. Sasa katika hali hiyo, tunajikuta katika wakati mgumu kwamba tunameiba mafuta wakati siyo kweli," anasema.

Mwakisyala anasema, kulazimishwa kupima mafuta kwa mita, kipimo ambacho wao madereva hawaziamini ni changamoto nyingine, akidai kuna uwezekano mkubwa wa 'kuzichezea' zisiwe na vipimo sahihi.

"Ukweli ni kwamba tunaumia sana na jinsi tunavyofanyiwa, halafu tunajikuta tunalipishwa gharama ambazo hatuhusiki kabisa. Ndio maana, tunaomba serikali iingilie kati kutoa kauli kuhusu vipimo hivi," anasema.

**WAZIRI VIWANDA**

Waziri wa Viwanda na Uwekezaji, Joseph Kakunda, anachangia hoja hiyo, akiahidi ataangalia uwezekano wa kukutana na madereva wa malori wote kuzungumza nao kwa kina, hatimaye kurekebisha kasoro yao.

"Wizara yangu ndio yenye dhamana katika hilo, kutokana na ukweli kwamba Wakala wa Vipimo wapo chini ya wizara hii. Hivyo, jambo la kufanya kukutana na viongozi wao na kuweka ratiba ya kukutana na wanachama wote na ikiwezekana wawepo pia wamiliki wa malori," anasema Kakunda.

Hata hivyo, anagusia vipimo vinavyotakiwa kutumika ni vya mita na siyo 'stiki' kama wanavyotaka madereva, na kwamba atakapokutana nao atatoa ufafanuzi unaostahili.

Anasema nchi za Tanzania, Kenya na Uganda, zinatumia vipimo vya mita kwa vile ndivyo vya kimataifa, hivyo ni muhimu madereva wavitambue na kuvitumia, kwani ndivyo vinavyoaminika.

"Kuchezewa mita ni suala lingine, ambalo nalo linatakiwa kuzungumzwa kwa kina, ili kama kweli kuna mchezo huo, basi ukomeshwe mara moja na hatimaye kuondoa manung'uniko haya," anasema.

Kakunda anasema kukutana na madereva hao, ni lazima amshirikishe Waziri wa Uchukuzi, kwani naye ana nafasi kwenye jambo, hilo ili alitolee maoni.

"Uzoefu unaonyesha kuwa kukiwa na jambo la kuzungumza kuhusu changamoto za madereva, mara nyingi wanaokuja wamiliki wa malori, sasa sitaki yatokee hayo ila kama watakuja basi wawe na madereva," anasema.

Waziri anasema madereva ndio wanaojua changamoto wanazokutana nazo kazini, hivyo wanapojitokeza wamiliki wa malori, hawawezi kujua hali halisi. Hivyo, ni vyema wakafika wote atakapitisha kikao.

Waziri anasema, iwapo watafika wote itakuwa rahisi kusikiliza changamoto hizo na kuzipatia ufumbuzi wa kudumu, lakini anahitimisha kwa kuhimiza, "utaratibu wa kupima mafuta kwa mita ni wa muhimu."

FEDHA >> USD 2,300.97| Pauni 2,979.53| Euro 2,575.48

BIASHARA

# Mtihani wa kinamama kufikia '50 kwa 50' katika ujasiriamali

- Shinyanga katika makusudi yanayowatoa machozi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA.

KUNA vilio na malalamiko ya matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wafanyabiashara wanawake kwenye masoko mbalimbali nchini, kuhusiana na ukiukwaji wa staha ya mwanamke. Ni mada isiyo na ugeni katika maandiko ya jarida hili.

Soko la Shinyanga Mjini, linanyooshewa kidole kuangukia na maeneo ya lugha chafu, udhalilishaji maungo ya mwanamke, kulazimishwa uhusiano wa kimapenzi na dhuluma za pesa.

Gazeti la Nipashe, limezungumza na wadau mbalimbali, kuanzia walio huru, wanaodai kuonewa na watoa maamuzi na ikapata ufafanuzi wao.

Baadhi ya masoko ya Shinyanga Mjini yanayotajwa si salama ni: Soko kuu, Nguzo Nane, Ibinzamata, Kambarage, Majengo Mapya, Ngokolo Mitumbani, pna Ndembezi.



Kinamama wakiendesha biashara zao katika Soko la Kambarage, mjini Shinyanga.

**WAHUSIKA WANENA**

Merysiana Shija, mfanyabiashara katika soko la Ndembezi mjini Shinyanga, analalamika kuwa miongoni mwa wanaokabiliwa na matukio hayo ya ukatili wa kijinsia, kwa kuonewa na kutolewa lugha chafu za matusi.

Anawataja wahusika ni wafanyabiashara wenzao wanaume na baadhi ya wateja, hasa wanaofika kuhudumiwa chakula.

Merysiana anatoa mfano, kuna wakati alikuwa anahudumia chakula kwa tenda kwa vibarua ambao waliwahi kugoma kumlipa na badala wake, akaambulia matusi.

"Kwa kweli wafanyabiashara wanawake tunanyanyasika sana kwenye masoko," analalamika mfanyabiashara huyo na kufafanua:

"Tunatukanwa matusi ya nguoni kwa kutajwa nyeti zetu, vipigo, kushikwashikwa maumbile bila ya ridhaa yetu, kudhulumiwa fedha na hata kushuka kiuchumi kwa sababu ya kuonekana sisi ni viumbe dhaifu."

Anadelea na simulizi: "Mfano, kwenye biashara yangu ya awali ya umamalishe, niliachana nayo, mara baada ya mtaji 'kukatika.'

"Nilikuwa nikilisha watengenezaji wa barabara kwa tenda, lakini baada ya kazi yao kwisha waligoma kunilipa huku nikiambulia matusi juu ya nguoni, nikaamua kuanza upya kwa biashara nyingine."

> **Ukatili huu wa kijinsia kwenye masoko dhidi ya wanawake unapaswa kupigwa vita, wakati mwingine unatushusha kiuchumi**

Mwingine mwenye simulizi ya mfano huo ni Agnes Giligili, kutoka Soko la Ngokolo Mitumbani, anayesema mwaka jana alishawahi kutukanwa matusi ya nguoni na mfanyabiashara mwezake mwanamume, anyeuza matunda,

Anasimulia ni mkasa uliomfanya afunge biashara kwa muda kutokana na kujihisi amehalilishwa kupita kiasi na msingi wa msuguano ni alipodai pesa yake.

Mama huyo anaendeleza simulizi kuwa, baada ya kupokea matusi hayo, huku mkasa huo ukikusanya umati, ilimfanya ajisikie aibu na akarudi nyumbani kupumzika.

Anaendelea kueleza kwamba, kutokana na tendo hilo, kijana huyo alijihisi kukosea na amlifuata nyumbani kwake na kumuomba msamaha kwa kitendo hicho kilichomdhalilisha, ndipo anakiri nafsi yake iliridhika.

"Ukatili huu wa kijinsia kwenye masoko dhidi ya wanawake unapaswa kupigwa vita, wakati mwingine unatushusha kiuchumi.

Mfano nilipofunga biashara yangu, tayari nilikosa kipato kwa siku au mtu anapodhulumiwa fedha zake, lazima arudi nyuma tu kimaendeleo," anasema Agnes.

**MWANAUME AFUNGUKA**

Anthony Sabuni, ni mfanyabiashara wa kiume kwenye Soko la Ngokolo Mitumbani, anayekiri wanawake kufayiwa ukatili huo wa kijinsia.

Anaainisha sababu za wenzake wa jinsia kutenda hivyo, ni ukosefu wa elimu ya ukatili na kuna baadhi wanaoyafanya hayo, pasipo kujitambua. Sabuni anasema:

"Unajua wafanyabiashara wote wa kiume siyo kwamba wanafahamu nini maana ya ukatili wa kijinsia. Mfano, lugha hizi za matusi ya nguoni na kushikashika wanawake maumbile yao, kwenye masoko vinaonekana tu ni jambo la kawaida, kumbe huo ni ukatili tena mkubwa sana.

"Kinachopaswa sasa ili kutokomeza ukatili huu kwenye masoko yote ya Shinyanga Mjini, ni utolewaji elimu ya kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia na kuainishwa matendo yapi yana ashiria ukatili, ili watu wapate kuyafahamu na kuachana nayo."

**WENYEVITI MASOKO**

Mwenyekiti wa Soko la Ngokolo Mitumbani, Trasy Leonard, anasema mara badaa ya kuona matukio hayo ya ukatili wa kijinsia yanazidi sokoni, walilazimika kuitisha kikao na viongozi wenzake na kuamua kutunga kanuni inayopiga marufuku udhalilishaji wa aina hiyo.

Leonard anataja baadhi ya vipengele ni kwa anayemtukana

INAENDELEA UK.20



Mamalishe wa Shinyanga, akiwa kazini. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# Mtihani wa kinamama kufikia ‘50 kwa 50’ katika ujasiriamali

INATOKA UK.19

mwezake akiwa sokoni, pasipo kujali jinsia anatozwa faini ya Sh. 5,000 au kufungiwa kufanya biashara kwa wiki mbili au vyote kwa pamoja.

“Kwenye soko letu hili, tumekuwa tukipambana sana kupinga matukio ya ukatili wa kijinsia, dhidi ya wafanyabiashara wanawake, ambao wao ndio ‘wahanga’ wakubwa wa kutolewa lugha za matusi ya nguoni, kushikwa maumbile yao na hata kudhulumiwa fedha.

“Pia tumepiga marufuku wanawake kuvaa nguo fupi (vimini) ambazo zimekuwa zikisababisha kwa namna moja au nyingine kufanyiwa ukatili, kwa kushikwa maumbile yao na hata kutakiwa kimapenzi kwa nguvu,” anaeleza mwenyekiti huyo.

Alex Stephen, Mwenyekiti wa Soko Kuu la Shinyanga Mjini, pia anakiri kukithiri vitendo vya ukatili wa kijinsia, wakatunga kanuni ndogo kwamba mtu akitoa lugha za matusi atatozwa faini ya Sh. 15,000 na kufungiwa biashara kwa wiki mbili.

Anasema kanuni hizo ndogo kwa kiasi kikubwa zimesaidia kupungua vitendo hivyo vya ukatili wa kijinsia sokoni na eneo ambalo linaonekana halijakomboka ni kwa baadhi ya wateja wa kiume kuwafanyia ukatili mamalishe, pindi wanapoenda kudai fedha za chakula.

**OFISA USTAWI**

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa ya Shinyanga, Bestina Gunje, anawataka kinamama wafanyabiashara hao wa masoko, inapotokea wanafanyiwa udhalilishaji huo wa kijinsia wasikae kimya, bali watoe taarifa kwa viongozi, ili wasaidiwe kisheria.

Anatoa mfano, wanadhulumiwa malipo yao, wanapaswa kutoa taarifa mapema kwa viongozi wa soko, au Manispaa ya Shinyanga na Dawati la Jinsia la Polisi, ili hatua zichukuliwe.

“Nimesikitika sana kusikia taarifa hii ya mamalishe ambaye alidhulumiwa fedha zake na vibarua waliokuwa wakitengeneza barabara na kuamua kukaa kimya, hatimaye kukatika mtaji wake na kuanza biashara nyingine,” anasema Gunje

“Angefika kwetu, sisi ambapo tungeweza kumsaidia kupata haki yake na asingeshuka kiuchumi,” anasema.

**MWANASHERIA**

Mwanasheria wa kujitegemea, Martha Masalu kutoka kampuni ya Masalu Law Attorneys ya mjini Shinyanga, anasema ukatili wa aina yoyote kijinsia ni kosa kisheria na kuna vipengele vinavyokataza utoaji wa lugha chafu na kushika maumbile ya mwanamke pasipo ridhaa yake.

Mustapha Isabuda, ni Ofisa miradi wa shirika la Agape mkoani Shinyanga, wanaotetea haki za watoto na wanawake, anasema wamechukua jukumu la kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa kinamama wafanyabiashara wa masoko ya Shinyanga Mjini.

Anasema, hilo linatokana na utafiti mdogo walioufanya mwaka jana kwenye Masoko ya Shinyanga Mjini, wakagundua idadi kubwa ya wafanyabiashara wanawake wanafanyiwa ukatili wa kijinsia, pasipo kujitambua na wapi pa kudai haki zao.

Isabuda anasema, matokeo ya utafiti wao ndio uliwafanya waona waanzishe mradi wa kutokomeza ukatili huo wa kijinsia, dhidi ya wafanyabiashara wanawake kwenye masoko ya Shinyanga Mjini chini ya kivuli cha shirika la kijinsia la Umoja wa Mataifa, liitwalo UN Women.

**AGAPE**

Helena Daudi ni Ofisa Mradi wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia kwa Wafanyabiashara Wanawake Sokoni, kutoka shirika la Agape, ana usemi ‘Mpe riziki siyo Matusi.’

Anasema mradi huo unaoendesha vita sokoni, ni mradi utakaodumu hadi Oktoba mwaka huu.



HABARI KITAIFA

# Serikali yatoa bil. 670/- ujenzi Stieglers

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Tanzania, imetoa dola za Marekani milioni 309.659 (sawa na takriban Sh. bilioni 688.650), zikiwa fedha zake za ndani kama malipo ya awali kwa mkandarasi Arab Contractors ya Misri, wanaojenga mradi wa kuzalisha umeme unaotokana na maporomoko ya maji ya Mto Rufiji, mkoani Pwani.

"Haijapata kutokea katika historia ya nchi hii Serikali kutoa fedha nyingi za malipo ya awali ya kiasi kama hiki cha Sh. bilioni 688.65 katika mradi wa aina yoyote uliowahi kutekelezwa hapa nchini isipokuwa huu," alisema Doto James, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango jijini Dar es Salaam juzi.

James, ambaye pia ndiye Mlipaji Mkuu wa Serikali, alimkabidhi hundi kifani ya dola za Marekani milioni 309.65, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dk. Hamisi Mwinyimvua, ambaye alimkabidhi hundi hiyo Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Ugavi wa Umeme nchini (TANESCO), Dk. Alexender Kyaruzi, ambaye pia alimkabidhi hundi hiyo Naibu Mkurugenzi wa Ujenzi wa mradi huo. Mhandisi Mohamed Hassan, kwa niaba ya kampuni za Arab Contractors (Osman A. Osman & Co na Elsewedy Electric S.A.E (AC-EE JV).

Alisema kiasi kilichotolewa cha Sh. bilioni 688.65 ni sawa na asilimia 70 ya zaidi ya Sh.trilioni 1 ya malipo ya awali yanayotakiwa kutolewa ya asilimia 15 ya mradi huo ambao hadi kukamilika kwake ndani ya miaka mitatu ijayo, unakadiriwa utagharimu zaidi ya Sh. trilioni 6.6.

James alizitaja baadhi ya faida za mradi huo utakapo kamilika na kuzalisha megawati 2,115 za umeme kuwa ni pamoja na nchi kuwa na umeme wa kutosha na wa uhakika, kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta ya viwanda vitakavyo chochea uzalishaji wa bidhaa, ajira pamoja na upatikanaji wa maji ya uhakika katika maeneo yanayozunguka mradi na mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

"Ninamtaka mkandarasi akamilishe mradi huu kwa wakati na kama ilivyokubaliwa kwenye mkataba ili mradi utakapo kamilika uwe kichocheo muhimu cha kuiwezesha Tanzania kufikia azma yake ya kuwa na uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025," alisisitiza James.

Kwa upande wake Dkt. Mwinyimvua, alifafanua kuwa kwa mujibu wa kifungu Na. 14.2 cha Mkataba, malipo ya awali ya Mkandarasi ni asilimia 15 ambazo zimegawanywa katika sehemu mbili ambapo asilimia 70 zinalipwa kwa kutumia sarafu ya kigeni (dola za Marekani 309.645m) na asilimia 30 zitalipwa kwa fedha za ndani ambazo zitalipwa baada ya Mkandarasi kukamilisha taratibu za kimkataba zinazohusu malipo hayo.

"Ninao uhakika kwamba malipo haya ya awali yatamwezesha Mkandarasi kukamilisha taratibu za kupeleka vifaa katika eneo la mradi na kuanza ujenzi mara moja kwa mujibu wa mkataba," alisema.

Naye, Dk. Kyaruzi, alisema uzalishaji wa umeme hapa nchini umefikia megawati 1,600 na kwamba kuongezeka kwa megawati nyingine 2,115 ni hatua kubwa na ya furaha na alimshukuru Rais John Magufuli kwa uamuzi wake wa kutekeleza mradi huo.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Mkandarasi wa mradi huo, Mhandisi Mohamed Hassan, alishukuru serikali na wananchi kwa ushirikiano mkubwa wanaoupata na amewahakikishia Watanzania kwamba mradi huo utatekelezwa kwa haraka na kwa viwango ili kutimiza matarajio ya nchi ambayo ni maendeleo.



Wauza matunda wakisubiri basi kuelekea kwenye sehemu zao za biashara katika kituo cha Buguruni sokoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

*Salamu za Pongezi*

MIAKA 55 YA MUUNGANO WA TANZANIA



1964 - 2019

Menejimenti na Wafanyakazi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), tunaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli na Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein na Watanzania wote katika kuadhimisha miaka **55** ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar




Dkt. John Pombe Magufuli
Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania

Mkurugenzi Mtendaji
Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF
S.L.P 2719 Dodoma
Simu + 255 26 2963866 Nukushi + 255 26 2963871
Barua pepe: info@tasaf.go.tz
Tovuti: www.tasaf.go.tz



Dkt. Ali Mohamed Shein
Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

215195302





# Marufuku watoto kubeba mizigo sokoni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UONGOZI wa Soko Kuu la Majengo jijini Dodoma, umepiga marufuku watoto chini ya miaka 18 kufanya kazi za kubeba mizigo na atakayekamatwa sheria kali zitachukuliwa dhidi yake pamoja na wazazi wake.

Marufuku hiyo ilitolewa jana na mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama ya soko hilo, Salumu Hamisi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanyika uchaguzi wa umoja wa wabeba mizigo.

"Naomba nitoe rai kwa wazazi wenye watoto wenye umri wa chini ya miaka hiyo ambao wengi wamekuwapo hapa sokoni wakifanya kazi ya kubeba mizigo ya wateja pamoja na kushusha bidhaa kwenye magari ni marufuku kufanya kazi hiyo, na atakayebainika tutamkamata," alisema. Alisema agizo hilo ni sehemu ya maelekezo yaliyotolewa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ambaye aliagiza watoto chini ya miaka hiyo ni marufuku kujihusisha na ubebaji wa mizigo ndani ya soko hilo.

"Hawa watoto wanatakiwa kwenda kusoma katika shule yao iliyopo Kigwe na hii kazi ya ukuli sio sehemu yao, hivyo basi atakayeonekana kwanzia leo hii tutamkamata na wazazi watawajibika katika hili," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Umoja huo sokoni hapo, Msafiri Joseph, alisema kuundwa kwa umoja huo kutasaidia kuimarisha usalama wa mizigo na wateja. Joseph alisema pamoja na kuimarisha usalama wa mali za wateja, pia umoja huo utautumia kuanzisha miradi mingine ambayo itawasaidia kujikwamua kiuchumi.

"Kutokana na kukosa umoja katika kipindi cha nyuma kulisababisha hata haki zetu za msingi kuzikosa, lakini pia wakati mwingine hata mwenzetu anapokuwa mgonjwa tunashindwa kumsaidia, hivyo umoja huu utatusaidia kujikwamua kiuchumi kwa kupata mikopo pamoja na kuwezeshana wenyewe kwa wenyewe," alisem Joseph.



Mkuu wa wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mnkunda, akishiriki zoezi la upandaji miti kwenye eneo linalojengwa hospitali ya wilaya hiyo, mkoani Dodoma jana, ikiwa ni maadhimisho ya miaka 20 ya Compassion. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC atoa angalizo tishio la njaa

**Na Elisante John,** SINGIDA

KUTOKANA na tishio la ukame kwa baadhi ya maeneo hapa nchini, serikali mkoani Singida imetoa angalizo kwa wananchi wake kuhakikisha wanajiwekea akiba ya kutosha ya chakula baada ya mavuno ya msimu huu, ili kutosheleza mahitaji yao kwa mwaka mzima.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, alisema hayo juzi wakati wa ibada ya umoja wa makanisa iliyofanyika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kati, usharika wa kiaskofu Imanuel, na kuhudhuriwa na waumini wa madhehebu 12 ya umoja huo.

Akizungumza na maelfu ya waumini hao, Dk. Nchimbi aliwaomba viongozi wa dini katika Mkoa wa Singida kuhimiza waumini wao na jamii kwa ujumla kutunza chakula kitakachotosheleza familia zao kwa kipindi chote cha mwaka.

"Kuna mazoea yaliyojengeka eti Singida ni kame, hilo siyo kweli!, Singida yetu siyo kame kabisa, Singida hii ni njema tena njema sana...hapa ukilima kila zao linastawi katika hali ya ubora na hata ukifuga, mifugo nayo inaboreka na kukuingizia fedha za kutosha," alisisitiza.

Aidha, Dk. Nchimbi aliiomba jamii kusimamia malezi bora kwa watoto wao ili baadaye kujenga kizazi chenye uthubutu wa kufanya kazi mbalimbali kwa ajili ya kujiletea maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Alisisitiza pia juu ya malezi bora kwa familia, na kuendeleza hali ya utulivu, upendo na amani nchini, tabia ambayo iliasisiwa na waasisi wa taifa hili, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Shekhe Amani Abeid Karume.

Kwa upande wake Paroko wa Kanisa Katoliki, Parokia ya Mandewa Singida Mjini, Padri Paterini Mangi, akisoma ujumbe wa Maaskofu wa Jumuiya ya CCT Tanzania, alisema familia zinapaswa kulikaribisha neno la Mungu ili kujiimarisha katika maisha yao ya kiroho na kimwili, hali itakayowezesha kukabiliana na changamoto za uvivu, matumizi ya dawa ya kulevya na ufinyu wa kufikiri katika kuanzisha miradi yao ya kiuchumi.

Aliitaka familia kuhudumiwa kwa upendo na kufundisha watoto wao maadili mema ili baadaye waje kuwa watu watakaojenga taifa imara, wenye kufuata maadili bora na chachu kwa maendeleo ya kanisa na jamii kwa ujumla.

# Vijana sasa wanolewa ujasiriamali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

VIJANA zaidi 30 wameanza kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali na stadi za maisha kupitia mradi wa Vijana Jiandalie ajira unaofadhiliwa na Shirika la Master Card la Marekani kupitia taasisi inayojishughulisha na masuala ya vijana ya International Youth Foundation (IYF).

Akizungumza wakati wa kuanza kwa mafunzo hayo jijini hapa, Ofisa Malezi wa kibiashara wa Taasisi ya Ujasiriamali na Ushindani Tanzania (TEEC), ambao ni waendeshaji wa mafunzo hayo, Mwasiti Mkembe, alisema vijana hao watapata mafunzo kuhusu ujasiriamali na stadi za maisha.

Alisema taasisi hiyo imekuwa ikiendesha program ya vijana jiandalie ajira ambayo inaundwa na taasisi tatu ikiwamo sekta binafsi, Taasisi ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Tume ya Sayansi na Teknolojia.

Alisema TECC inafanya kazi katika mikoa minne ya Dar es Salaam, Mtwara, Pwani na Dodoma.

Alisema kuwa TEEC kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido), wanatoa mafunzo ya ujasiriamali na stadi za maisha ili vijana waweze kujisimamia katika biashara zao.

Alisema katika mafunzo hayo wamechukua vijana wa kuanzia umri wa miaka 18 hadi 24 ambao watapatiwa mafunzo ya siku kumi kuhusu namna ya kuanzisha biashara zao na kuzisimamia.


Mmoja wa wanufaika wa mafunzo yanayotolewa na TEEC, Consensa Mushi, alisema alipata mafunzo kama hayo miaka miwili iliyopita na sasa anaweza kusimamia biashara zake ambazo zinamsaidia kuendesha maisha.

"Wakati naanza ilikuwa mwaka 2017 wakati huo nikisoma katika Chuo Kikuu cha Dodoma Kitivo cha Elimu na baada ya mafunzo nilianza kufanya biashara ya nguo nikiwa chuoni" alisema.

Alisema baada ya kumaliza chuo alianza kutengeneza vitafunwa na kufungasha dagaa na juisi, na kwamba biashara hizo zilimuwezesha kupanga chumba na kuanza kujitegemea.

Alisema wakati huu akisubiri ajira, amekuwa akiendelea kufanya biashara kwa kusambaza vitafunwa kama karanga za mayai, tambi, chips na ubuyu na sasa amenunua friji kwa ajili ya kuuza soda na juisi

Alisema alianza akiwa na mtaji wa Sh. 30,000 na sasa mtaji wake umefika Sh. 500,000 na faida yake ya biashara zake kwa mwezi ni Sh. 200,000.







Wauza magazeti wakiwa wamejipumzisha kando ya Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, eneo la Mbuyuni, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: JOHN BADI**

# Wananchi watakiwa kuwa jasiri kutaja wala rushwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wametakiwa kujenga tabia ya ushujaa na kutoa taarifa za rushwa kwa taasisi husika kwa lengo la kukomesha vitendo hivyo ambavyo hudhoofisha maendeleo.

Ofisa kutoka Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumi Uchumi Zanzibar (ZAECA), Yussuf Juma, alisema jamii haina mwamko katika kupambana na rushwa.

Akizungumza katika mafunzo kuhusu mradi wa majaribio wa kupingana na misimamo mikali na kupiga vita rushwa na uhujumu uchumi, Ofisa huyo alisema kuwa tatizo la woga limekuwa ni changamoto kubwa kwa wananchi, hivyo wameamua kutoa namba ambayo itawezesha kutuma ujumbe au kupiga simu ili kutoa taarifa za rushwa.

Alisema watu wamebakia kuzilalamikia taasisi mbalimbali katika masuala ya rushwa, lakini hakuna mtu aliyekuwa tayari kufichua vitendo vya rushwa.

"Tatizo la rushwa na kero yake haiwezi kumalizika bila ya jamii yenyewe kuibua na kufichua suala hilo kwa kutoa taarifa katika vyombo husika vya sheria," alisema.

Alieleza zipo njia mbalimbali za kutoa taarifa za rushwa kwa ZAECA ikiwamo namba za mawasiliano ya simu.

"Zipo njia mbalimbali za kufikisha taarifa za mapambano ya rushwa kwa jamii, tena kwa harama...ipo namba 113 ambayo wananchi wanaweza kuitumia kufikisha ujumbe haraka wa rushwa," alifafanua zaidi.

Mratibu wa mafunzo hayo, Mohamed Jaffar kutoka Kenya, alisema changamoto zinazowakabili wananchi wengi katika mapambano dhidi ya rushwa ni ushirikiano mdogo kutoka vyombo vya sheria.

Alisema vyombo vya sheria vinatakiwa kuongeza ushirikiano ikiwamo kutoa elimu kwa wananchi zaidi wa vijijini ambao hawafahamu taratibu na njia za kutoa taarifa kuhusu rushwa. Alieleza mradi huo wa majaribio wa kupinga misimamo mikali na masuala ya rushwa utaendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini kwa lengo la kufikisha ujumbe huo.

"Vyombo vya sheria vinatakiwa kutoa elimu zaidi kuhusu masuala ya rushwa, lakini pia kujenga ushirikiano na vyombo vya habari katika kutoa elimu ya rushwa kwa jamii," alisema.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walivitaka vyombo vya ulinzi ikiwamo Jeshi la Polisi kuongeza ushirikiano katika kutokomeza rushwa.

# Wizara yanunua CT-scan ya mamilioni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imetiliana saini mkataba wa ununuzi wa mashine mpya ya CT-scan na kampuni ya Pacific Diagnostic Ltd ya Dar es Salaam yenye thamani ya dola laki nane.

Mkataba huo umehusisha ununuzi, uletaji, ufungaji pamoja na utoaji wa mafunzo ya CT-scan kwa watendaji wa Wizara ya Afya. Mkurugenzi Mkuu Wizara ya Afya, Dk Jamala Adam Taib, alisema kuwa kupatikana kwa mashine hiyo mpya ya CT-scan ni hatua kubwa ya mafanikio kwa Zanzibar ambayo itasaidia wananchi katika kuchunguza maradhi mbalimbali.

Alisema serikali imeona ipo haja ya kununua mashine hiyo mpya kwa sasa kutokana na kuongezeka kwa huduma mbalimbali za afya zinazotolewa nchini ambazo zinahitaji uchunguzi wa kina na wa haraka katika hospitali.

Alisema mashine hiyo itakuwa na uwezo mkubwa wa kiteknolojia ukilinganisha na iliyopo sasa katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, ambayo imedumu kwa miaka 10.

Alieleza fedha zilizotumika kununulia mashine hiyo ni za serikali kwa asilimia 100, na kwamba ni juhudi kubwa zinazochukuliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, za kuhakikisha sekta ya afya inakuwa kwa kiwango kikubwa na wananchi wanapata huduma zenye ubora.

Dk. Jamala alisema tangu kuanza kwa hatua ya kuwapo kwa mashine ya CT-scan kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja, kumesaidia kuwapo huduma nyingi ikiwamo kuja kwa madaktari wa magonjwa ya kichwa na mgongo kutoka nje ya nchi ambao wanasaidiana na madaktari wazalendo katika kuwapatia matibabu nchini.

Kwa upande wake, Mwakilishi kutoka Kampuni hiyo, Brian Kamuzoka, alihakikishia serikali kuwa mashine ambayo wataileta ni yenye ubora na inatumika katika hospitali kubwa duniani.

Alisema baada ya kuifunga mashine hiyo watakuwa na mkataba maalumu wa kuifanyia matengenezo pamoja na kuisimamia ili kufanya kazi zake kwa ufanisi.

# Tamwa yataka Polisi kusaka mtuhumiwa mauaji ya mwanamke

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, (TAMWA) ofisi ya Zanzibar, kimelitaka Jeshi la Polisi kumtafuta na kumkamata mtuhumiwa wa kesi ya mauaji ya Eliza Juma John (30), yaliyotokea Mpapa, Wilaya ya Kati Unguja.

Tukio hilo la kikatili liliripotiwa Aprili 21, mwaka huu ambapo inadaiwa kuwa Lucas Tabu Mshoni, mume wa marehemu kuwa ndiye aliyetenda kosa hilo.

Mkurugenzi wa Tamwa Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema, Tamwa imeshtushwa sana na tukio hilo la kikatili.

Alieleza kuwa taarifa za awali zilizopatikana kuhusiana na tukio hilo zinadai mtuhumiwa wa mauaji hayo ambae inasemekana ni mumewe, alimfungia chumbani baada ya kumuua na kukimbia kusikojulikana.

"Habari zinasema kuwa Eliza alikufa takriban siku nne nyuma kwani alipobainika mwili wake tayari ulisha haribika... ni wapita njia ndiyo waliosikia harufu na kupeleleza ndani ya nyumba waliyokuwa wakiishi yeye na mumewe, "alisema Dk. Mzuri. Hata hivyo, alisema TAMWA, Zanzibar inategemea Jeshi la Polisi kutumia uwezo wake wote kumsaka mtuhumiwa ili aje apambane na vyombo vya sheria, hivyo kuwataja wote wanaofanya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Alieleza kuwa kesi za mauaji zimekuwa zikichukua muda mrefu na mara nyingi waliotenda vitendo hivyo hukimbia, hivyo kukwepa adhabu wanazostahili.

Dk. Mzuri alilishauri Jeshi la Polisi kuimarisha vitengo vyake na miundombinu ya upelelezi kwa sababu hali hii inajenga hofu sana kwa raia hasa wanawake na watoto ambao hawana nguvu za kujilinda dhidi ya mashambulizi.

"Vitendo vya ukatili wa kujeruhi vibaya na mauaji vimekuwa vikiongezeka hasa katika Mkoa wa Kusini Unguja ambapo kuanzia mwaka 2016 wanawake wanane na watoto wapatao wawili wameuliwa," alisema.

Akizungumzia kuhusu tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, Hassan Suleiman, alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi ili kumtia mbaroni mtuhumiwa wa mauaji hayo.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Friday**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Iljimae
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Night of terror
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Series rpt: Iljimae
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 ShambÅa shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Documentary
22:00 Kipindi Maalum: Tatu mzuka
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Kipindi Maalum: TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY**
05:30 Uwanja wa Ma0zoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Illegal sisters
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Illegal sisters 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)

## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

| TIME | MONDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

| TIME | TUESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | WEDNESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | THURSDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | FRIDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | SATURDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

| TIME | SUNDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

# Majaji wajiunga na maandamano Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

KWA mara ya kwanza tangu kufanyika maandamano ya nchi nzima Sudan, majaji nchini humo wamesema wataungana na waandamanaji nje ya makao makuu ya jeshi, kulihamasisha jeshi kukabidhi madaraka kwa serikali ya kiraia.

Taarifa kutoka kwa kundi la majaji inasema majaji hao wanatarajiwa kuanza maandamano yao nje ya mahakama ya katiba hadi katika makao makuu ya kijeshi, kuunga mkono mabadiliko yanayotakiwa ya kuwa na mahakama zenye uhuru.

Wakati huohuo, viongozi wa maandamano hayo wametishia kuandaa maandamano ya taifa zima iwapo watawala wa kijeshi hawatoridhia matakwa yao ya kurejesha utawala wa kiraia.

Hata hivyo baraza hilo la kijeshi linaloshikilia madaraka limesema limewaalika viongozi wa maandamano kwa mazungumzo katika ikulu ya rais.

Awali wakati wa mkutano na waandishi wa habari kiongozi mkuu wa upinzani alisema viongozi wa maandamano wanatarajiwa kukutana ana kwa ana na Mkuu wa Baraza la Kijeshi, Abdel Fattah al-Burhan.

"Tuko tayari kuzungumza na jenerali Burhan na nadhani masuala yetu yatatatuliwa kupitia majadiliano," alisema kiongozi huyo wa upinzani Omar el-Digeir alipokuwa akizungumza na waandishi habari.

Wiki iliyopita viongozi wa maandamano ya kutaka mabadiliko ya kidemokrasia na kisiasa nchini humo walisema wameyaahirisha mazungumzo yao na baraza la kijeshi baada ya kudai kuwa linaendeleza matakwa ya serikali iliyopita iliyoongozwa na rais aliyepinduliwa madarakani, Omar Hassan al Bashir.

Jeshi lilimuondoa al-Bashir madarakani baada ya miezi kadhaa ya maandamano dhidi ya utawala wake wa kidikteta.

Maelfu ya waandamanaji wamekuwa wakipiga kambi nje ya makao makuu ya jeshi mjini Khartoum, wakitaka viongozi wapya wa kijeshi kukabidhi madaraka kwa serikali ya kiraia.

Waandamanaji hao wanaungwa mkono na Marekani inayotaka pia jeshi likabidhi mara moja madaraka kwa serikali ya kiraia.

Lakini hapo jana viongozi wa kiafrika waliokusanyika nchini Misri katika mkutano ulioitishwa na Rais Abdel Fattah al-Sisi, walilisisitiza haja ya Sudan kupewa muda zaidi wa miezi mitatu kwa jeshi hilo kukabidhi madaraka.

Hata hivyo, Umoja wa Afrika (AU) Aprili 15 ulitishia kuiondoa Sudan katika Umoja huo iwapo itashindwa kukabidhi madaraka hayo ndani ya muda wa siku 15.

**DW**




Polisi nchini Sri Lanka wakiwa wameimarisha doria katika maeneo yaliyotokea milipuko, ambapo hadi jana idadi ya watu waliofariki ilifikia 356. **PICHA: REUTERS**

# Rais Tshisekedi kutangaza serikali mpya muda wowote

**KINSHASA,** Congo

BAADA ya kukabidhiwa madaraka miezi mitatu iliyopita, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Félix Tshisekedi ameahidi kwamba hivi karibuni atatangaza serikali mpya.

Rais Tshisekedi ametoa kauli hiyo akiwa ziarani mjini Kisangani, katika Jimbo la Tshopo mwanzoni mwa wiki ikiwa ni sehemu ya ziara yake Kaskazini mashariki mwa nchi hiyo, ili kutathmini miradi ya maendeleo nchini humo.

Hali hiyo imekuja siku moja baada ya kukutana kwa mazungumzo na mtangulizi wake, Joseph Kabila yaliyohusu uteuzi wa waziri mkuu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na ikulu ya rais jijini Kinshasa, Rais Tshisekedi alienda Kisangani kuzindua miradi ya maendeleo ikiwamo ukarabati wa miundombinu kama barabara pamoja na kuanzishwa upya kwa ujenzi wa madaraja mawili kwenye Mito ya Lubunga na Wanyarukula,

Katika taarifa kwa vyombo vya habari, serikali ya jimbo la Tshopo ilisema kuwa Rais Tshisekedi alizindua rasmi daraja kubwa la Lubuya lenye urefu wa mita 30, kwenye mto Wanyerukula ulioko kilomita 54 kutoka mji wa Kisangani kwenye barabara ya Lubutu.

Daraja hilo linaunganisha mikoa ya Maniema na ule wa Tshiopo, na ni muhimu kwa kurahisisha shughuli za kibiashara.

Inaelezwa kuwa ujenzi wa daraja hilo umefadhiliwa na serikali kupitia Mfuko wa Kukuza Viwanda (FPI) ikitarajiwa kuwa litaunganisha mikoa ya kivu Kaskazini na Kusini, Maniema na Tshopo miaka 50 baada ya kuporomoka kwake.

**RFI**

# Sri Lanka yafanya mabadiliko vikosi vya usalama

**COLOMBO,** Sri Lanka

RAIS wa Sri Lanka, Maithripala Sirisena, amefanya mabadiliko katika vikosi vya usalama zikiwa zimepita siku tano tangu kutokea kwa milipuko ya mabomu kipindi cha Pasaka yaliyosababisha vifo vya watu zaidi ya 350 nchini humo.

Sirisena amefanya uamuzi huo baada ya maafisa kushindwa kuchukua hatua licha ya kupokea taarifa za onyo la uwezekano wa kutokea mashambulizi.

Maafisa wa upelelzi wa Sri Lanka walionywa na India saa kadhaa kabla ya kutokea mashambulizo hayo. Lakini haijulikani iwapo maafisa hao walichukua hatua yoyote kufuatia onyo hilo.

Katika hotuba ya televisheni aliyoitoa usiku wa Jumanne, Rais Sirisena alisema atambadilisha mkuu wa vikosi vya majeshi katika kipindi cha saa 24.

Hata hivyo, Rais Sirisena alisema alifichwa taarifa hizo za uwezekano wa kutokea mashambulizi na ameahidi kuchukua hatua kali dhidi ya maafisa wote walioshindwa kumuarifu mapema.

"Kuna mjadala unaendelea na watu wanaulizana kwanini vikosi vya usalama vya nchi hii havikuchukua hatua yoyote baada ya kupata taarifa za onyo kutoka nchi jirani. Lazima niseme kwamba mimi sikuarifiwa kuhusu onyo hilo na maafisa husika. Ningeliarifiwa, basi ingewezekana kuchukua hatua za haraka," alisema Rais Sirisena.

Upande wa upinzani nchini humo unapingana na kauli ya Rais Sirisena na kusema kwamba baraza la usalama, waziri mkuu na rais mwenyewe pamoja na baraza la mawaziri wote walikuwa wanazo taarifa hizo hata kabla ya mashambulizi hayo kutokea.

Mmoja wa wanasiasa wa upinzani, Keheliya Rambukwella, katika mkutano na waandishi habari alisema kwamba serikali kukaa kimya ulikuwa ni uamuzi wa kisiasa.

"Nadhani ulikuwa ni uamuzi wa kisiasa, walihisi hawapaswi kuwatikisa hawa viongozi wa Kiislam, kwa sababu ya kuogopa kukosa kura za waumini wao, na wananchi ndiyo walioumia, pamoja na takriban wageni 40," alisema Rambukwella.

Polisi wa Sri Lanka walisema wamewakamata watu wengine 18 wanaowashuku kuhusika na mashambulizi hayo ya Jumapili ya Pasaka, huku idadi ya vifo ikiwa imeongezeka na kufika watu 359.

Kundi linalojiita Dola la Kiislam IS limekiri kuhusika, baada ya maafisa wa Sri Lanka kusema walijitoa muhanga kwa kujilipua walilipiza kisasi cha mashambulizi ya misikiti miwili ya New Zealand ya mwezi Machi yaliosababisha vifo vya watu 50.

**DW**

# Kesi ya Wambura yapigwa kalenda kisa mgonjwa

**Na Elizabeth Zaya**

ALIYEKUWA Makamu wa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Michael Wambura, ambaye anakabiliwa na kesi ya utakatishaji fedha, ameshindwa kufika katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, kwa sababu ni mgonjwa.

Taarifa hiyo ilitolewa jana kutoka gereza la Segerea mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Kelvin Mhina, wakati shauri hilo lilipopelekwa kwa kutajwa.

Kesi hiyo ilipotajwa mshtakiwa hakuwapo mahakamani ndipo Hakimu Mhina alipouliza upande wa askari Magereza ambapo walidai kwamba alishindwa kufika kwani ni mgonjwa.

Baada ya kudai hayo, Hakimu Mhina aliahirisha kesi hiyo hadi Mei 9, mwaka huu kwa kutajwa.

Awali, Wakili wa Serikali, Ester Martin, alidai shauri hilo lilipelekwa kwa kutajwa na upelelezi wa shauri hilo bado unaendelea hivyo anaomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Wambura anakabiliwa na mashitaka 17 yakiwamo ya kutakatisha fedha.

Mshtakiwa yuko rumande kutokana na mashtaka yanayomkabili kutokuwa na dhamana.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, mshtakiwa anadaiwa Julai 6, mwaka 2004, sehemu isiyojulikana ndani ya Jiji la Dar es Salaam, alighushi barua ambayo haina kumbukumbu akionyesha imeandikwa na E Maganga ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Jeck system anadai kurejeshewa malipo ya mkopo wa USD 30,000 pamoja na riba aliyokuwa ameikopesha TFF.

Vile vile inadaiwa siku hiyo aliwasilisha nyaraka ya uongo, alitoa barua iliyokuwa haina kumbukumbu namba ya Julai 6, 2004, akijifanya kwamba ni barua iliyoandikwa na E. Maganga ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Jeck System Ltd, akionyesha kuwa anadai mkopo wa USD 30,000 pamoja na riba waliokopeshwa TFF huku akijua kuwa siyo kweli.

Shtaka la tatu hadi 15 mshitakiwa anadaiwa kujipatia kiasi cha zaidi Sh.milioni 95, kwa njia ya udanganyifu akidai kuwa fedha hizo ni sehemu ya malipo ya jumla ya kiasi cha fedha mbalimbali na riba kutoka kwa Kampuni ya Jeck System Ltd huku akijua kuwa siyo kweli.

Katika shtaka la utakatishaji fedha, Wambura anadai kati ya Agosti 15 na Oktoba 21, mwaka 2014, Makao makuu ya Shirikisho hilo, alijipatia Sh. milioni 25 kutoka TFF huku akijua fedha hizo ni zao la kosa la kughushi.

## Mashahidi wakwamisha kesi ya Malinzi

**Na Elizabeth Zaya**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na utakatishaji fedha, inayomkabili aliyekuwa Rais wa Shirikishi la Soka Tanzania (TFF), Jamal Malinzi na wenzake wanne, imeshindwa kuendelea na usikilizwaji kwa sababu mashahidi ambao waliwategemea kutoa ushahidi wana udhuru.

Washtakiwa hao walipanda kizimbani jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Maira Kasonde, wakati shauri hilo lilipopelekwa kwa ajili ya kuendelea na usikilizwaji ambapo Jamhuri ilitarajiwa kuendelea kutoa ushahidi wake.

Mwendesha Mashtaka kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(TAKUKURU), Leonard Swai, alidai kuwa shauri lilipelekwa kwa kuendelea na ushahidi upande wa Jamhuri ambapo tarehe iliyopita waliwapa barua ya wito mashahidi ili waende kutoa ushahidi, lakini hawajafika kwa sababu tofauti.

"Shauri lilitakiwa kuendelea na usikilizwaji, lakini leo hatuna shahidi ambapo wiki iliyopita tuliwapa barua ya wito wote wana udhuru kwani wamesafiri na wengine ni wagonjwa, hivyo tunaomba tarehe fupi," aliiomba mahakama.

Baada ya kudai hayo, Wakili wa Utetezi, Richard Rweyongeza, alidai hana pingamizi na hilo ila anaomba shauri hilo lipangiwe tarehe ya karibu akidai kuwa imekaa muda mrefu.

Hakimu Kasonde baada ya kusikiliza maelezo ya pande zote mbili, aliahirisha kesi hiyo hadi Aprili 30, mwaka huu kwa ajili ya kuendelea na usikilizwaji.

Tayari mashahidi 13 wa upande wa jamhuri wameshatoa ushahidi dhidi ya Malinzi akiwamo aliyekuwa dereva wake.

Mbali na Malinzi aliyekuwa Rais wa (TFF), washtakiwa wengine ni aliyekuwa Katibu Mkuu wa TFF, Selestine Mwesigwa; Mhasibu wa TFF, Nsiande Mwanga,; Meneja wa TFF Miriam Zayumba na karani, Flora Rauya.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashitaka 30 katika kesi ya jinai namba 213 ya mwaka 2017 yakiwamo kughushi, kula njama, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na utakatishaji Dola za Marekani 173, 334.

Kabla ya Hakimu Kasonde shauri hilo lilikuwa mbele ya Hakimu Wilbard Mashauri, ambaye aliteuliwa na Rais John Magufuli kuwa Jaji wa Mahakama Kuu, hivyo kesi hiyo imepangiwa kwa Hakimu Mkazi Maira Kasonde.

Malinzi, Mwesigwa na Nsiande wako rumande kwa kukabiliwa na mashtaka ya utakatishaji wa fedha ambayo ni miongoni mwa mashtaka ambayo kwa mujibu wa sheria, hayana dhamana, huku wenzao Miriam na Flora wakiwa nje kwa dhamana.



Vijana wakisafisha mazingira kwa kuondoa nyasi zilizoota katikati ya tuta la Barabara ya Mandela, eneo la Ubungo Riverside, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

INATOKA UK 8

## Serikali yatoa maagizo mazito

taarifa ya uwezekano wa kimbunga hicho kuyakumba maeneo yao.

Shughuli mbalimbali za kibinadamu pia ziliendelea kusimama huku serikali ikitangaza mapumziko kwa wafanyakazi na wanafunzi ili kutoruhusu athari kutokea dhidi yao.

Nipashe ilishuhudia jana wananchi wa Mkoa wa Mtwara wakilazimika kukusanyika maeneo maalum yaliyotengwa kwa tahadhari ambayo ni Uwanja wa Ndege Mtwara, Shule ya Sekondari Sabasaba na maeneo mengine ili kujiepusha na athari zinazoweza kusababishwa na kimbunga hicho.

Katika maeneo hayo wanawake na watoto wao, wazee walionekana wakiwa ni miongoni mwa wengi walioacha makazi yao na kwenda kujihifadhi sehemu salama.

Tangu asubuhi ya jana, hali ya hewa mkoani humo ilikuwa ikibadilikabadilika na mvua ziliendelea kunyesha huku Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, akieleza kuwa kadri kimbunga hicho kinaposogea mvua, zitaongezeka zaidi.

Dk. Kijazi alisema kimbunga hicho kitadumu kwa siku mbili hadi Jumamosi na tofauti na vimbunga vingine, kitatua nchi kavu na kurudi baharini.

"Wakati mwingine kimbunga kinapotua nchi kavu kinapotea lakini hiki kitarudi baharini, kikirudi baharini tunaomba wananchi waendelee kufuatilia taarifa za TMA ili kujua kimerudi eneo gani na kama kitaleta athari ukanda wetu au la," alisema.

Dk. Kijazi alisema endapo kitadumu eneo la Msumbiji, ni dhahiri kuwa na Tanzania iendelee kuchukua tahadhari.

Alisema kimbunga hicho kitakuwa na upepo wa kilomita 140 baharini na zitafika kilomita 170 na kitakapotua nchi kavu kitakuwa kilomita 100 kwa saa.

"Kilomita 100 kwa saa ni kazi kubwa ya upepo ambayo inaweza kusababisha athari nyingi," alisema.

Alisema kimbunga hicho ni cha kwanza chenye nguvu kinachoelekea Pwani ya Msumbiji na kuleta athari Tanzania.

Dk. Kijazi, akielezea kitaalam hali ilivyokuwa Mtwara kupitia picha ya satelaiti jana mchana, alisema kimbunga hicho kilikuwa kimekaribia kuelekea mpakani mwa Tanzania na Msumbiji.

Alisema wamefuatilia katika mifumo yote ya hali ya hewa na kuona kitaleta athari baadhi ya maeneo hasa ya kusini mwa nchi.

Dk. Kijazi alisema hadi majira ya saa tisa alasiri jana, kilikuwa kimefika latitudo 11.9 kusini na longitudo 40.2 mashariki.

Alisema eneo hilo lina umbali wa 177 kutoka maeneo ya Mtwara na kitaongezeka nguvu hadi kilometa 140 kwa saa.

"Utabiri unaonyesha hadi kufika kesho (leo) alfajiri, kitatua maeneo ya Pwani ya Msumbuji takribani latitudo 12.3 kusini, longitudo 39.4 mashariki na hali hii ni sawa na kilometa 237 kutoka Pwani ya Mtwara," alisema.

"Ni muhimu kwa sasa wananchi waendelee kufuatilia taarifa hizi na kuchukua hatua kulingana na maelekezo, kwa sababu yapo maeneo ambayo yameelekezwa waende, mvua tangu asubuhi ya leo (jana) zimenyesha, wasione ni mvua ndogo kwa sababu kadri kimbunga kinavyokuja na mvua zitaongezeka zaidi."

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, alitangaza mapumziko kwa wafanyakazi na wanafunzi huku watumishi wengine kwenye taasisi za afya, polisi na Shirika la Umeme (Tanesco) wakitakiwa kuendelea na utekelezaji wa majukumu yao.

MELI, BOTI

Wakati huo, Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (Tasac) limetoa tahadhari kwa wamiliki na manahodha wa vyombo vya usafiri wa majini, likiwataka kuegesha vyombo vyao ili kusalimisha maisha ya watumiaji na mali kwa ujumla.

Kaimu Mkurugenzi wa Tasac, Japhet Loisimaye, alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa ni vyema kuzingatia tahadhari iliyotolewa na TMA kuhusu kimbunga hicho.

"Nasi tumeamua kuweka msisitizo kwa kuwa mojawapo ya jukumu la Tasac ni kuhakikisha vyombo vyote vya majini vinakuwa salama," alisema Loisimaye.

"Tunawasihi wananchi kuwa wavumilivu kwa siku hizi tatu, wasije kufikiri ikipita Aprili 26 (leo) inayohofiwa kuwa na madhara hayo zaidi kwamba hali itakuwa shwari, bali inabidi kuongeza siku mbili zaidi kujiridhisha ndipo waendelee na shughuli zao."

Kamishna wa Operesheni wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Billy Mwakatage, katika taarifa yake jana, alisema wamejipanga na wako imara kuhakikisha wanatoa huduma bora, sahihi na kwa wakati wote wa tukio la kimbunga hicho.

"Wananchi wanatakiwa kuchukua tahadhari katika kipindi hiki na kuendelea kufuatilia taarifa za utabiri kutoka TMA na kusikiliza vyombo vya habari ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza," alisema.

Pia alisema kutokana na kimbunga hicho kikali kinachoambatana na mvua kubwa, kuna uwezekano wa mawe makubwa au udongo kuporomoka milimani au miti kuanguka na kuziba barabara hivyo madereva watumiaji wengine wanapaswa kuchukua tahadhari.

***Imeandikwa na Hamis Nasri (Mtwara), Godfrey Mushi (DODOMA), Romana Mallya na Beatrice Mosses (DAR)**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311**


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUCIANA WILFREDY MKONGWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 772 DDS DAIHATSU.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KJN/RB/762/2019.**

115196302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AKIL MURTAZA HEMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 359 AKM TOYOTA HARRIER.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KJN/RB/762/2019.**

115197002

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

MUSSA G. SHEYO ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA HIACE YENYE NAMBA ZA USAJILI T 822 AAA.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI
**MB/RB/6234/19.**

115196802

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## HATI YA KIAPO

Mimi SELEMANI RAJABU S.L.P 178, Tanga, mtu mzima nathibitisha yafuatayo;

1. Kwamba mimi ni msimamizi wa mirathi Na.18/2019 ya marehemu SELEMANI MFAUME.
2. Kwamba hati ya toleo (Offer of the right of occupancy, L.O Nos 18833) iliyotolewa tarehe **10/12/1957** imepotea. **TAN/RB/3310/2019.**
3. Kwamba naziomba mamlaka za Ardhi kunipa hati nyingine ya umiliki kwa jina la marehemu **SELEMANI MFAUME.**

**MBELE YA: R.S MHINA**
**CHEO: HAKIMU**

115196702

## IN THE COURT OF DISTRICT DELIGATE OF DODOMA AT DODOMA

**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO.36 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late GODFREY D. KAULA- DECESEASD**

**And**

**In the matter of Application for letters of Administration by DANIEL KAULA AND MARIAM HASSAN- PETITIONER**

**GENERAL CITATION**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before 22ND /05/2019.

Dated at Dodoma this ….24/04/2019

Resident Magistrate
DODOMA

115196902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JUMA M. MASEPELE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA FUSO YENYE NAMBA ZA USAJILI T 667 ADB.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI:
**MB/RB/6227/2019.**

215196602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FORTUNATUS MAKORE MAGAMBO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA IST yenye namba za usajili T 265 CRW. Chassis namba NCP600172125, Engine namba 2NZ3388425.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DOM/TR/RB/2544/2018.**

115196502


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*



**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



# Hazard, Real Madrid wakaribia kumalizana

**LONDON,** England

NYOTA wa Klabu ya Chelsea, Eden Hazard, anakaribia kukamilisha usajili wa ndoto yake kwa kujiunga na Real Madrid baada ya taarifa kudai kwamba 'Los Blancos' hao wanatarajia kutangaza ofa yao ya mshahara.

Hazard amebakiza msimu mmoja tu kwenye mkataba wake wa sasa na Chelsea na hana mpango wa kusaini mkataba mwingine.

Na hilo ndilo linaloifanya Chelsea kufanya maamuzi ya kumuuza kwenye kipindi cha majira ya joto kwa kuepuka kuondoka hakiwa huru mwakani.

Iliripotiwa mapema mwezi huu kwamba, Real ilipanga kutoa ofa ya pauni milioni 85 kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo na Gazeti la Marca limedai kwamba tayari klabu hiyo imetoa ofa ya euro milioni 100 kumsajili.

Hata hivyo, taarifa zaidi zinaeleza kwamba, Chelsea watamruhusu tu Hazard kuondoka kama Real Madrid watakuwa tayari kulipa kiasi cha euro milioni 100.

Gazeti hilo limelezea kuwa Hazard hataki kushinikiza mazungumzo yake, huku Chelsea ikipigania kushinda Kombe la Europa, lakini Real imejipanga kikamilifu kuhakikisha inamsajili mwishoni mwa msimu huu.

Kwa mujibu wa Gazeti la Sun, ofa ambayo Madrid ipo tayari kutoa ni kumlipa pauni 400,000 kwa wiki, huku akitia mfukoni pauni milioni 20 kwa mwaka, pamoja na bonasi ya ziada ya pauni milioni 15.

Imebainishwa kwamba Real ipo tayari kuongeza kiasi zaidi cha fedha ili kumtwaa Hazard.



# GUARDIOLA: UBINGWA EPL BADO KWA CITY

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amewaonya wachezaji wake kuendelea kutulia kwa ajili ya kumaliza mechi zao tatu zilizobaki kama wanataka kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England.

Man City ilikaribia ubingwa huo baada ya juzi Jumatano kuwafunga wapizani wao wa jiji moja, Manchester United kwa mabao 2-0 kwenye dimba la Old Trafford, shukrani kwa mabao ya kipindi cha pili ya Bernardo Silva na Leroy Sane.

City sasa inaongoza msimamo wa Ligi Kuu kwa pointi moja zaidi ya Liverpool na ushindi dhidi ya Burnley, Leicester na Brighton utatosha kuwafanya wanyanyue kombe hili ndani ya wiki tatu zijazo, lakini Guardiola amewaonya wachezaji wake kuwa makini.

"Bado sisi si mabingwa, kuna mechi tatu zimebaki," alisema raia huyo wa Hispania wakati akizungumza na BBC Sport.

"Nimewaambia wachezaji watulie, wasiangalie televisheni, wanatakiwa kulala na kupumzika kwa ajili ya mchezo dhidi ya Burnley.

"Tunatakiwa kwenda kucheza na Burnley na tunajua kwamba utakuwa mchezo mgumu. Ni muhimu sisi kutulia."

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 48, ndoto yake ya kutwaa mataji manne msimu huu ilimalizwa na Tottenham baada ya kuwatoa kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wiki iliyopita, lakini bado wanaweza kushinda mataji matatu.

Huku Guardiola akijisikia kwenye wakati mzuri wa kuizuia Liverpool kushinda ubingwa wake wa kwanza wa Ligi Kuu tangu mwaka 1990.

Alibainisha: "Timu zote zinastahili kutwaa ubingwa, lakini inaweza kuwa mara moja tu.

"Timu ambayo inakwenda kupoteza haiwezi kujutia kwa sababu yeyote atakayecheza kwa ubora wake ndiye atashinda."

# Eriksson: Sijaomba kazi kuinoa Scotland



**LONDON,** England

KOCHA wa zamani wa England, Sven-Goran Eriksson, hajawahi kufikiria kuhusu suala la kuwa kocha wa timu ya Taifa ya Scotland.

Raia huyo wa Swedenameripotiwa kwamba aliomba kazi ya kuwa kocha wa timu ya taifa ya nchini hiyo kupitia FA, ili kuchukua mikoba ya Alex McLeish, ambaye alifukuzwa wiki iliyopita.

Hata hivyo, kocha huyo mwenye umri wa miaka 71, ambaye alimaliza nafasi yake ya kuwa kocha wa muda wa Ufilipino Februari mwaka huu, amesema hana mkataba nao.

Wakati alipoulizwa kuhusu nafasi hiyo, Eriksson aliiambia BBC Sport: "Sijui, sijawahi kufikiria kuhusu hilo."

Eriksson, ambaye alizifundisha timu kama Benfica, Lazio, Manchester City na timu ya Taifa ya Ivory Coast kwa kipindi chake cha miaka 42 ya ukocha, aliiongoza Ufilipino katika ushindi mara mbili katika mechi zake 10 alizoifundisha.

Aliipeleka England robo fainali ya Kombe la Dunia mwaka 2002 na 2006 na michuano ya Ulaya 2004.

## HABARI MICHEZO

# Real Madrid yajitosa usajili wa Jadon Sancho

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane amemuweka kwenye orodha Jadon Sancho katika mbio zake za kutaka kumsajili mwishoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England, amekuwa mmoja wa nyota ambao wanang'ara Ulaya kwa sasa akiwa katika msimu wake wa pili katika Klabu ya Borussia Dortmund, akifunga mabao 12 na kutoa pasi za mwisho 18 katika mashindano yote.

Sancho amekuwa akihusishwa kwa muda mrefu kurudi kwenye Ligi Kuu ya England kwa kipindi cha miaka miwili baada ya kuondoka Manchester City, lakini Gazeti la Bild limeripoti kwamba, Real Madrid sasa imejiunga kwenye mbio za kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19.

Kocha mkuu, Zidane ameripotiwa kwamba anamuwania Sancho na 'Los Blancos' hao wameambiwa kwamba atawagharimu kiasi cha euro milioni 180 ambapo itakuwa rekodi kwa klabu ya Real Madrid.

Sancho alijiunga na Borussia Dortmund kwa ada ya euro milioni saba mwaka 2017, lakini tayari amecheza mechi 51 katika kikosi cha kwanza.

Bao lake la hivi karibuni ni dhidi ya SC Freiburg na alimpita Christian Pulisic kwa mabao katika Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Real Madrid imekuwa ikihusishwa na usajili wa vijana kama vile, Vinicius Junior, Brahim Diaz na Rodrygo ambao kwa pamoja waliigharimu kiasi cha euro milioni 107.







# SOLSKJAER ABWATUKA KIPIGO MAN CITY

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer, amewabwatukia wachezaji wa Manchester United kwamba wanamuangusha kwa kushindwa kutimiza majukumu yao uwanjani.

Solskjaer kwa sasa amepokea kipigo mara mbili mfululizo kwenye Ligi Kuu England baada ya kutoka kufungwa mabao 4-0 kutoka kwa Everton na kupokea maumivu ya kufungwa 2-0 nyumbani mbele ya Manchester City juzi usiku.

Matokeo hayo yamemfanya akasirike na kuwavaa nyota wake wanne ambao anawalaumu kwa kushuka ghafla kiwango ndani ya kikosi hicho.

Chris Smalling, Ashley Young, Nemanja Matic, Romelu Lukaku hawa ndio wapo kwenye mstari mwekundu wa kupigwa chini ili aanze kusuka kikosi kipya cha mauaji huku Paul Pogba ikiripotiwa kwamba amewaambia wachezaji wenzake anataka kusepa.

Kocha huyo aliteuliwa kufundisha kwa muda timu hiyo, Desemba mwaka jana ambapo alipata matokeo mazuri mwanzoni na wachezaji kuonekana kujituma. Hata hivyo, upepo uligeuka ghafla baada ya kupewa mkataba wa kudumu, Machi 28, mwaka huu.

"Tulionyesha kiwango chetu na mwisho wa siku tukafungwa na timu bora," alisema Solskjaer akiiambia Sky Sports.

"Lakini tulipata mrejesho kutoka kwa mashabiki na wachezaji na tulitakiwa kupigana mwanzo mwisho, lakini kama unavyoweza kuona wachezaji hawakuwa kwenye kiwango chao.

"Kuna tofauti kwenye ubora. Ndio maana wao wapo juu na sisi tupo hapa tulipo. Walitengeneza ubora wa kwenye daraja la juu. Kuishi Manchester hakukufanyi uwe bora. Ni suala la kuziba pengo lililopo."

# Arsenal nne bora inawezekana- Emery

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery, amesisitiza kwamba kikosi chake kinaweza kupata nafasi ya kumaliza nne bora kwenye Ligi Kuu England, licha ya kufungwa mabao 3-1 na Wolves Jumatano.

Ruben Neves, Matt Doherty na Diogo Jota ndio walifunga mabao hayo katika kipindi cha kwanza kwa kikosi hicho cha Nuno Espirito Santo, huku Sokratis Papastathopoulos akiwafungia 'Washika Bunduki' hao wa London.

Kipigo hicho kimekiacha kikosi cha Emery sasa kikiwa nafasi ya tano, pointi moja nyuma ya Chelsea, lakini Mhispania huyo anaamini kwamba wana ubora wa kutosha kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.


"Tulikatishwa tamaa, lakini tunahitaji kukumbuka wapi tulikuwa miezi mitatu iliyopita," alisema akiiambia BBC Sport.

"Hatuwezi kukatishwa tamaa na matokeo haya, kwani tunatakiwa kupigana kuhakikisha tunamaliza kwenye nne bora.

"Tulijua kabla ya mchezo kwamba, ungekuwa ni mgumu kwa sababu Wolves wana kikosi imara.

"Walilinda vizuri lango na wana wachezaji ambao wana uwezo wa kushambulia na hivyo ndivyo ilivyotokea, tulizidiwa na wakatufunga."






# SOLSKJAER AMKUBALIA KEANE POGBA KUMHARIBIA UNITED

**Manchester,** England

KOCHA Ole Gunnar, Solskjaer, amesema anaheshimu maoni ya nahodha wa zamani wa Manchester United, Roy Keane baada ya kipigo cha mabao 2-0 nyumbani kutoka kwa mahasimu wao, Manchester City.

Mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Bernardo Silva na Leroy Sane, huku makosa ya David de Gea yakielezwa kuhusika, yaliiwezesha Man City juzi kuibuka na ushindi huo katika Uwanja wa Old Trafford.

Akichambua mchezo huo kupitia Sky Sports, Keane alimulika kiwango cha United, huku akimkosoa kiungo Fred kwa "kudanganya" na kudai wachezaji ndio waliomtupa Jose Mourinho chini ya basi na wanaweza kulifanya hilo pia kwa Solskjaer".

Aidha, kabla ya mchezo huo pia Keane alipuuzia maoni ya kiungo Paul Pogba aliyoyatoa katika mkutano na wanahabari kuelekea mechi hiyo ya Manchester 'dabi' na kumtuhumu nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa kwa kucheza kwa ajili yake binafsi.

Pogba ambaye alikuwa katika kikosi cha kwanza kilichokubali kipigo cha mabao 4-0 dhidi ya Everton Jumapili kwenye mechi ya Ligi Kuu, kabla ya mechi ya juzi dhidi ya City, katika mahojiano yaliyorekodiwa na Sky Sports alinukuliwa akisema United lazima ionyeshe moyo wa kupambana baada ya kupoteza mechi sita kati ya nane ilizocheza kwenye mashindano yote.

"Siamini maneno aliyosema, hakuna maana kwa hili," alisema Keane.

> **"Kama unakwenda kuwa mchezaji mwenza mzuri unapaswa kurudi nyuma na kuzuia. Walisema ilikuwa hasira dhidi ya Everton – nasikia wapaka nywele mafuta kila mmoja."**

Pogba, ambaye alitwaa mataji manne mfululizo ya Serie A akiwa na Juventus, alikuwa nguzo muhimu kwa Ufaransa wakati ikitwaa Kombe la Dunia na Keane hapingi kipaji chake.

"Ni kijana mwenye kipaji, lakini tumemuona harudi nyuma," alisema. "Ni mchezaji kijana ambaye ameshinda mataji makubwa na sidhani kwamba anaongoza kwa mfano kutoka kile nilichokiona.

"Ukweli ni mwenye kipaji, lakini unahitaji zaidi ya kipaji. Mchezaji wa kweli wa kiwango cha juu anaifanya timu yake na wachezaji wenzake kuwa bora. Hakuweza kufanya hilo. Anacheza kwa ajili yake."

Hata hivyo, Solskjaer amekubaliana na maoni hayo ya Keane akisema atakisafisha kikosi cha United mwishoni mwa msimu wakati huu sasa kikiwa kimepoteza mechi saba kati ya tisa zilizopita kwenye mashindano yote huku wakiwa nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi.

"Na Roy mara zote nimekuwa na uhusiano mzuri naye," Solskjaer alisema katika mkutano wa wanahabari baada ya mechi dhidi ya City. "Na, unaweza kusemaje, ninathamini maoni yake sana na nimepata maoni yake.

"Tumecheza pamoja kwa miaka mingi na ni mtu wa Man United. Na hiyo ni kazi yangu kuhakikisha kwamba wakati nitakaporudi baada ya maandalizi ya msimu mpya ninakuwa na watu sahihi ndani na wanaozunguka [kikosi]. Kwa sababu hilo kamwe halitaruhusiwa."

## KWA UFUPI

### RONALDO KUMKUBALI GUARDIOLA JUVE

MSHAMBULIAJI wa Juventus na Ureno, Cristiano Ronaldo, 34, atakaribisha uteuzi wa kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, kuwanoa mabingwa hao wa Serie A. (Marca)

### VAN DIJK ANUKIA TUZO YA PFA

BEKI wa Liverpool na Uholanzi, Virgil van Dijk, 27, anajiandaa kutangazwa kuwa Mchezaji Bora wa Mwaka wa Kulipwa EPL (PFA) kwa kumpiku mshambuliaji wa Manchester City, Raheem Sterling, 24. (Evening Standard)

### WAKUTEMWA WAANDALIWA FUNGU UTD

MANCHESTER United imeandaa fedha za dharura kwa ajili ya kuwalipa wachezaji itakaowatema majira ya joto. (Sun)

### HAZARD KUTISHA MSHAHARA REAL

EDEN Hazard, 28, anajiandaa kupewa ofa ya kulipwa pauni 400,000 kwa wiki na Real Madrid katika mpango wa klabu hiyo kumshawishi kujiunga nayo akitokea Chelsea. (Sun)

### OBLAK KUMRITHI DE GEA

KIPA wa Atletico Madrid, Mslovenia Jan Oblak, 26, anaongoza katika orodha ya makipa wanaopewa nafasi ya kurithi mikoba ya mlinda mlango wa Manchester United, David de Gea, 28, endapo ataondoka Old Trafford. (Metro)

### HERRERA KUMSUBIRISHA SOLSKJAER

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, atakuwa mgonjwa katika suala la kusajili kiungo majira haya ya joto hadi atakapojua endapo nyota wa kimataifa wa Hispania Ander Herrera, 29, atabaki. (Teamtalk)

### ERIKSEN AZUA BUMBUAZI SPURS

TOTTENHUM inakabiliwa na bumbuazi endapo majira haya ya joto imuuze kiungo Christian Eriksen. Nyota huyo wa kimataifa wa Denmark mwenye umri wa miaka 27, amebakiza zaidi ya mwaka mmoja katika mkataba wake unaomfanya kulipwa pauni 75,000 kwa wiki na Real Madrid na Inter Milan zimekuwa zikimtupia jicho la karibu. (Mirror)

### WEST HAM, LEICESTER VITANI

West Ham na Leicester City zote zinavutiwa kumsajili winga wa AC Milan na Uturuki, Hakan Calhanoglu, 25, anayethaminishwa na pauni milioni 26. (Star)

### FLETCHER KUPEWA KAZI UNITED

KIUNGO wa Stoke na Scotland, Darren Fletcher, 35, ambaye atakuwa nje ya mkataba mwishoni mwa msimu, anaweza kurejea Manchester United katika majukumu ya kusaka vipaji. (Telegraph)

### MARTINELLI KIMEELEWEKA ARSENAL

ARSENAL imepanga tarehe muhimu kwa kinda wao mpya waliomsajili, Gabriel Martinelli, 17, ya kuanza kuichezea klabu hiyo kwa mara ya kwanza baada ya kukubaliana na Ituano katika dili la kumsajili mshambuliaji huyo raia wa Brazil. (Yahoo Brasil via Metro)

### CITY KUMFUYATA LUIS BENFICA

MANCHESTER City inataka kutoa ofa kwa kiungo mkabaji kinda wa Benfica, Mreno Florentino Luis, 19. (Guardian)

### MEUNIER BEI NAFUU SOKONI

BEKI wa kulia wa Klabu ya Paris Saint-Germain, Thomas Meunier, 27, raia wa Ubelgiji anatajwa kwamba anaweza kununuliwa kwa bei nafuu zaidi na Manchester United kama wakimhitaji. (Independent)

# KMKM WAZIMA NDOTO ZA KVZ UBINGWA Z'BAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Mabaharia wa KMKM, wamenyoosha njia yao ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya juzi kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi wapinzani wao wakubwa katika mbio hizo, Maafande wa KVZ.

Mabaharia wa KMKM kabla ya ushindi huo walikuwa wakiongoza ligi hiyo kwa tofauti tu ya mabao ya kufunga na kufungwa kufuatia kuwa na pointi 74 sawa na Maafande wa KVZ, lakini sasa kwa matokeo hayo ya juzi wamekaa kileleni wakiwa na pointi 77, tatu zaidi ya wapinzani wao hao.

Kwa matokeo hayo, sasa KMKM inahitaji pointi moja tu katika mechi yake ya mwisho dhidi ya JKU wakati KVZ wao ili kutwaa ubingwa wakilazimika kushinda zaidi ya mabao 30 Jumamosi dhidi ya Chuoni huku wakiombea mabaharia hao wapoteze Jumapili.

Hiyo ni kutokana na KMKM tofauti ya mabao yake ya kufunga na kufungwa kuwa 59 wakati KVZ tofauti yake ya mabao ikiwa ni 29.

Katika mchezo huo wa juzi uliopigwa dimba la Amaan majira ya saa kumi alasiri mabao ya KMKM yalipachikwa nyavuni na Brahamani Othmani Chinga dakika ya 57 huku la pili likifungwa dakika ya 86 kwa mkwaju wa penalti na Mudrik Muhibu baada ya mchezaji wa KVZ Iddi Mgeni kuunawa mpira ndani ya eneo la hatari.

Akizungumzia mchezo huo Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu alisema malengo yao yametimia ya kuhakikisha wananyakuwa ubingwa msimu huu na kudai kuwa KMKM itazidi kufanya maajabu hata katika msimu unaokuja.

Ligi hiyo inatarajia kuendelea tena Jumamosi kwa Mlandege kuvaana na Jang'ombe Boys Uwanja wa Amaan majira ya saa kumi alasiri, huku KVZ wakiwaalika Chuoni Uwanja wa Mau ze dong majira ya saa kumi alasiri na itafikia ukingoni Jumapili kwa KMKM kumenyana na JKU.




**WAYA...** Matt Doherty akiifungia Wolverhampton bao la pili kwa kichwa baada ya kipa wa Arsenal, Bernd Leno, kupoteza mwelekeo wa kuwahi kuucheza mpira wa juu kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa katika Uwanja wa Molineux juzi na Gunners kulala 3-1.
**HABARI UK. 29**

# Jang'ombe Boys, Pan African vitani Amaan Zanzibar leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BINGWA wa michuano ya Kombe la Muungano anatajiwa kujulikana leo kufuatia mchezo wa fainali utakaozikutanisha mabingwa watetezi wa kombe hilo, Jang'ombe Boys ya Zanzibar dhidi ya Pan African ya jijini Dar es Salaam katika Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Katibu wa Kamati ya Mashindano hayo, Kijo Nadir Nyoni, akizungumza na mwandishi wetu jana, alisema maandalizi kwa ajili ya mchezo huo yamekamilika na wanachosubiri kwa sasa ni kuwasili kwa Pan African ikitokea jijini Dar es Salaam Ijumaa asubuhi kabla ya jioni kushuka dimbani.

Alisema katika mchezo huo kiingilio kitakuwa Sh. 1,000 huku mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Diwani wa Kata ya Usaranga, Kimara jijini Dar es Salaam.

Alisema wanashukuru maandalizi yanaenda kama walivyopanga na kutoa shukrani zao kwa kamishna wa michezo Sharifa Khamis kwa kuwaunga mkono kwa kiasi kikubwa.

Awali kabla ya fainali hiyo walipanga kuchezwe mechi za mtoano ili kupatikane bingwa atakaecheza fainali hiyo, lakini ilishindikana kutokana na ratiba ya uwanja na timu ambazo walitarajia kuzijumuisha kubanwa na ratiba ya michezo yao.

Kutokana ugumu wa ratiba, wakaona ni bora mechi ya fainali kuchezwa moja kwa moja kati ya bingwa mtetezi wa kombe hilo, Jang'ombe Boys na mabingwa wa jijini Dar es Salaam, Pan African.

# Simba Queens yapania 'kuitoboa' JKT Queens

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

WAKATI mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania, JKT Queens, wanatarajia kuwakaribisha Simba Queens katika mchezo wa ligi hiyo utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo jijini Dar es Salaam, "ndugu wawili" wa jiji moja, Marsh Queens na Alliance Girls watavaana katika dimba la Nyamagana jijini hapa.

JKT Queens watashuka uwanjani kuwakaribisha Simba Queens huku wakiwa hawajapoteza mchezo hata mmoja katika ligi hiyo na wakiwa na kumbukumbu ya kupata ushindi finyu wa bao 1-0 dhidi ya 'Wekundu wa Msimbazi' hao katika mchezo wa mzunguko wa kwanza.

**Akizungumza na gazeti hili jana, nahodha na mshambuliaji tegemeo wa JKT Queens, Asha Rashid , alisema wamejiandaa kuendeleza ushindi, lakini wanafahamu mchezo huo hautakuwa mwepesi kutokana na wapinzani wao kuimarika.**

Asha alisema mzunguko wa pili wa ligi hiyo umekuwa na ushindani zaidi kutokana na timu kujiimarisha kwa kusajili wachezaji wapya ambao waliongeza nguvu katika vikosi vyao.

"Tunajua mechi haitakuwa rahisi kama ile tuliyocheza katika mzunguko wa kwanza, na si Simba Queens, mechi zote hazitabiriki siku hizi," alisema mshambuliaji huyo.

Naye nahodha wa Simba Queens, Mwanahamisi Omary, alisema wamejiandaa vema na wanaamini mechi ya leo ushindani utakuwa mkubwa zaidi.

Mwanahamisi alisema endapo watatumia vizuri nafasi watakazozitengeneza, wanaamini leo wanaweza kuweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza kuwafunga mabingwa hao watetezi wa ligi hiyo inayochezwa kwa mtindo wa nyumbani na ugenini.

Wakati huo huo, Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Mkoa wa Mwanza (MRFA), Leonard Malongo, aliliambia gazeti hili kuwa, maandalizi ya mchezo kati ya Marsh Queens na Alliance Girls yamekamilika na wanaamini wakazi wa jijini hapa watajitokeza kwa wingi kushuhudia vipaji vya mabinti zao.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo zitakuwa ni kati ya Panama FC dhidi ya Mlandizi Queens wakati Evergreen Queens watavaana na Tanzanite Queens huku Kigoma Sisterz wakiwakaribisha Mapinduzi Queens kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

# Michezo

Ijumaa Aprili 26, 2019

Nipashe

## Solskjaer abwatuka kipigo Man City



HABARI UK. 29

HUPITI...




Kiungo wa Manchester United, Nemanja Matic, akimdhibiti mshambuliaji wa Manchester City, Sergio Aguero, wakati wa mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Old Trafford juzi na wageni hao kushinda 2-0. **HABARI UK. 28**

# SIMBA YABAKIZA 8 ZA YANGA KILELENI

## Bocco, Okwi waishusha Azam nafasi ya tatu, waifuata Biashara United huku...

**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

SIMBA imeendelea kujiimarisha katika mbio za kuishusha Yanga kileleni kuelekea ubingwa wa Ligi Kuu Bara baada ya jana kuishusha Azam hadi nafasi ya tatu kufuatia kuichapa KMC FC mabao 2-1 katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini hapa.

Mabingwa hao watetezi sasa wamefikisha pointi 66 na kukaa katika nafasi ya pili nyuma ya vinara Yanga wenye pointi 74 kwenye msimamo wa ligi hiyo, lakini wakiishusha Azam FC kutokana tu na tofauti nzuri zaidi ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Kwa matokeo hayo, Simba imebakiza pointi nane tu kuifikia Yanga kileleni ambayo Jumatatu itakuwa na kibarua kigumu dhidi ya Azam katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Bao la kwanza la mabingwa hao watetezi lilipatikana dakika ya 20 kupitia kwa Mganda Emmanuel Okwi ambaye alipokea pasi fupi iliyoanzishwa na James Kotei baada ya kupiga mpira wa faulo.

Hassan Kabunda aliifungia KMC bao la kusawazisha baada ya kumzidi mbio Zana Coulibaly na kupiga shuti lililomshinda kipa Aishi Manula kudaka na kutinga wavuni moja kwa moja. Nahodha John Bocco aliifungia Simba bao la pili kwa njia ya penalti dakika ya 82 na kurejesha furaha kwa mashabiki wa Msimbazi ambao walikuwa wanadhani mchezo huo ungemalizika kwa sare kutokana na KMC kucheza kwa kuelewana zaidi katika kipindi cha pili.

Wasiwasi kwa mashabiki wa Simba ilizidi kufuatia awali Meddie Kagere kukosa penalti baada ya kupiga shuti dhaifu lililodakwa na kipa wa KMC, Jonathan Nahimana kutokana na refa Abdallah Kambuzi kutoa adhabu hiyo baada ya Okwi kumnawisha Ismail Gambo mpira akiwa ndani ya 18.

Simba ilienda mapumziko ikiwa mbele kwa bao 1-0 katika mchezo huo wa kiporo na wa tatu mfululizo kwa Simba ikiwa kwenye Kanda ya Ziwa.

Hata hivyo, walikuwa ni KMC FC wanaofundishwa na Mrundi Etienne Ndayiragije, ambao walianza kufanya shambulizi katika lango la Simba kupitia kwa Abdul Hillary lakini shuti lake liliishia mikononi mwa Manula dakika ya sita huku Yusuf Ndikumana akitoa nje kwa kichwa krosi iliyopigwa na Koulibaly na kuwanyima Wekundu wa Msimbazi nafasi ya kufunga dakika mbili baadaye.

Dakika ya 11 kipa wa KMC FC, Nahimana aliwahi kudaka mpira wa kichwa uliopigwa na Okwi ambaye aliunganisha krosi ya Clatous Chama na kupoteza nafasi ya kufunga huku Bocco akipiga shuti fyongo dakika ya 11 na kuharibu kazi nzuri iliyofanywa na Kagere.

Dakika ya 26, Simba ilipoteza nafasi nyingine ya kufunga baada ya Chama kupiga shuti nje akiwa amepokea pasi kutoka kwa Kagere na KMC FC wakajibu shambulizi hilo lakini straika wake, Hassan Kabunda alichelewa kuunganisha pasi ya Omary Ramadhani akiwa ndani ya eneo la 18.

Bocco alikosa nafasi ya wazi tena kwa shuti lake kugonga mwamba wa juu baada ya kupokea mpira ulioanzia kwa Chama na Kagere dakika ya 43, lakini Chama alichelewa tena kumalizia pasi iliyopigwa na Okwi dakika ya 52.

Kituo kinachofuata kwa Simba sasa ni mjini Musoma, Mara ambapo wataikabili Biashara United katika mchezo mwingine wa ligi hiyo utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Karume.

## Lyanga aingia rada za Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI klabu ikiwa katika mchakato wa maandalizi ya uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika ifikapo Mei 5, mwaka huu, Kamati ya Usajili ya Yanga imeanza mazungumzo na Coastal Union ili kumsajili mshambuliaji wa timu hiyo ya jijini Tanga, Ayoub Lyanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, mmoja wa viongozi wa Coastal Union ( jina tunalihifadhi), alisema klabu yao iko tayari kumuuza endapo Yanga itatoa kiasi cha fedha walichowaambia.

Kiongozi huyo alisema kuwa awali Yanga ilianza kuzungumza na mchezaji huyo, lakini baada ya kubaini kwamba bado ana mkataba na Coastal Union walilazimika kufuata utaratibu sahihi wa usajili.

"Yanga wanatusumbua sana kuhusu Lyanga, ila tumewaambia watupe pesa tu, maana kama washaona atawafaa, sisi tutawauzia na tutaendelea kutengeneza vijana wengine," alisema kiongozi huyo aliyepo ngazi za juu Coastal Union.

Alisema klabu yake inajivunia kutumia zaidi wachezaji vijana inaowapandisha kutoka katika kikosi cha pili na wamekuwa wakiwapa matokeo mazuri licha ya kukabiliana na changamoto mbalimbali kutoka kwa timu pinzani.

"Coastal Union bado inaamini vijana ndio wenye uwezo na watakaosaidia kufanya mapinduzi ya kupunguza nyota wa kigeni wanaokuja kubahatisha, timu yetu ina wachezaji wengi wa U-20, wanafanya vema na wanawasumbua hao wanaojiita wakongwe," aliongeza kiongozi huyo.

Hata hivyo, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, alinukuliwa mapema wiki hii akikataa kuanza mchakato wa usajili kwa madai kwamba klabu hiyo haina fedha kwa sasa.

Lakini kamati ya kuchangisha fedha iliyoko chini ya Mwenyekiti wake, Anthony Mavunde, inaelezwa kuwa na zaidi ya Sh. milioni 500 baada ya kukusanya pesa kupitia harambee waliyoifanya mapema mwezi huu jijini Dodoma kwa kuwaalika viongozi mbalimbali wanaoipenda klabu hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >